

Elimu Juu ya Pepo

Milki ya Kidini

 Sijui ni wangapi wanaufahamu wimbo huu mfupi, ninapowasalimu kwa salamu motomoto sana za ushirika wa Kikristo na upendo wa Kristo leo, ni wangapi wanaoufahamu wimbo huu mfupi, “Anakujali”? Mnaufahamu? Sawa, hebu tuone kama tunaweza. Unaufahamu, dada? Unaufahamu? Sasa:

Anakujali,
Anakujali;
Juani au kivulini,
Anakujali.

Loo, vizuri kabisa. Hebu tuujaribu tena sasa.

Anakujali,
Anakujali;
Juani au kivulini,
Anakujali.

² Baba yetu wa Mbinguni, [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.]...twaamini ya kwamba Wewe watujali na umedhihirisha upendo Wako kwetu, hata ukamtuma Mwanao Mwenyewe mpendwa, ku-...Mwana wa Mungu asiye na hatia, kuchukua mahali pa wenye hatia walio na dhambi. Jinsi tunavyokushukuru, ya kwamba Wewe ulitujali na ulitufikiria, kwa kutenda hili! Na tunafurahia sana jambo hilo, Bwana. Tuna furaha kukutanika hapa alasiri ya leo, chini ya paa la anga, na tunaomba baraka zako kwa ibada hii. Tujalie, Bwana, ya kwamba kila mwanamume, mwanamke, mvulana ama msichana aliyepo hapa, apate kujifunza Maandiko kwa undani sana. Tunakabili ulimwengu ambao unatawaliwa na Shetani. Na, Baba, tunaomba, tunapojifunza nguvu za pepo na mambo wanayowatendea watu, ya kwamba utatupa imani kubwa, na jalia ishara nyingi na maajabu yafanyike. Kwa kuwa, tunaomba katika Jina la Kristo na kwa utukufu wa Mungu. Amina.

³ Tunaninii, somo la alasiri ya leo, tutaliingilia upesi, nafikiri, kama dakika kumi na tano mapema. Lingali ni juu ya *Elimu juu ya Pepo*.

⁴ Na sasa nimepokea ujumbe sasa hivi, muda mfupi uliopita; Ndugu Beeler, toka kwa rafiki zangu. Basi nitaanzia Afrika, katikati ya Julai. Kwa hiyo hilo linamaliza kila kitu, sasa tumemaliza mambo. Naye Ndugu Baxter hataweza kwenda wakati huo, kwa hiyo itanibidi kwenda Afrika peke yangu. Kwa hiyo nikienda kule na...labda ninii...Yawabidi mniombee

sasa, kwamba Bwana atanisaidia, maana kweli nitayahitaji hayo sasa, huko miongoni mwa . . . Ninatarajia watu wasiopungua laki mbili kwenye mkutano huo.

⁵ Nami nina ono lililoandikwa hapa. Ninataka ninyi watu mfaidike nalo. Lilitokea Desemba. Nilikuwa chumbani asubuhi moja wakati Malaika wa Bwana alipoingia. Ni- . . . Unaona, nilipokuwa kule, sikumtii Mungu, nami nikapatwa na amiba. Mtu ye yote anajua—anjua amiba ni nini, ni kimelea kinachopata . . . karibu kikuue. Na kwa sababu nilifanya jambo ambalo Mungu aliniambia nisifanye. Ni wangapi waliosikia habari hiyo? Nafikiri baadhi yenu mko hapa. Ninajua watu walio karibu na maskani walisikia hicho kisa kilichotukia. Mungu aliniambia niende mahali fulani, na nisikaribie mahali *hapa*, na nirudi niende mahali pengine. Nami nikawaacha wahubiri wanishawishi nisiende. Sasa, wahubiri ni wazuri sana, nao ni ndugu zangu, lakini wewe jali yale Mungu anayokwambia. Hiyo ni kweli. Unaona? Una jukumu moja.

⁶ Ni wangapi wanakumbuka wakati mmoja kulikuweko na manabii wawili katika Biblia? Na mmoja wao, Bwana alimwambia, kasema, “Nenda mahali *fulani*. Wala usi—usije ninii. . . Rudi kwa njia nyingine,” na kadhalika. Na—na kasema, “Usile wala usinywe wakati ukiwa kule.”

⁷ Kisha nabii mwingine wa kweli akakutana naye, na akasema, “Bwana alikutana nami baada ya kukutana na wewe.” Basi akasema, “Njoo nyumbani kwangu.” Na huyo nabii akasikiliza yale yule mwingine aliyosema, akapoteza maisha yake kwa ajili ya jambo hilo. Unaona, unafanya yale Mungu anayokwambia ufanye haidhuru mtu mwingine ye yote anasema nini.

⁸ Sasa sisi tuna- . . . Katika ono hili, Yeye . . . Liliniamsha, tarehe kumi na tatu ya Septem- . . . ama ya Desemba. Na—na nilipokuwa nimeketi ukingoni mwa kitanda changu, nilikuwa nikijiuliza maisha yangu ya baadaye yatakuwaje. Niliporudi hapa, wao walikuwa tayari kunitupa kwenye wadi ya magonjwa ya kuambukiza, vimelea vilikuwa karibu kuniua. Nao wakanifanyia uchunguzi nilipofika humu nchini. Na, kwa neema ya Mungu, wakaniruhusu niende nyumbani, kwa sababu vimetawanyika sana. Nami nikaomba, na nikawaendea wale wahudumu, nikasema, “Bwana aliniambia nisipitie njia hiyo.”

Kasema, “Loo, Mungu ananena na mtu mwingine mbali na wewe.”

⁹ Nikasema, “Kora alikuwa na wazo hilo wakati mmoja.” Na kwa hiyo, lakini nilienda nikachukua majani kidogo nikayaweka kwenye miguu yao, na kusema, “Kumbukeni, katika Jina la Bwana, kama tukienda huko kwenye ziara hiyo, itakuwa ni kazi bure, na sote tutajuta.” Na kwa kweli tulijuta! Loo, jamani! Wote karibu tufe. Kwa hiyo basi tulipokuwa tunarudi . . .

¹⁰ Una mambo mengi sana ya kushindana nayo katika nchi hizo za kigeni. Kwa mfano, kioboto kidogo kingekuuma, na kingesababisha upatwe na homa ya kupe. Na kajitu hako kadogo, kanapokuuma, kama ukijisikia unawashwa, huwezi kukakuna. Unaangalia, kama ni kajamaa kadogo keusi, usikang’oe. Kana kichwa kidogo, kinapenya kwenye ngozi, kanageuka namna *hii* na kujikaza. Kama ukikang’oa, kichwa kitakatikia ndani. Kina kirusi, ambacho kingekulemaza. Kwa hiyo usijikune, wala usimvute atoke; chukua tu mafuta kidogo. Nacho huvuta pumzi kwa nyuma. Kimwagie mafuta, nacho kitatoka.

¹¹ Halafu kuna mbu mdogo. Hapigi kelele hata kidogo. Anapitia moja kwa moja hewani. [Ndugu Branham anapigapiga mkono wake—Mh.] Anakugusa tu, kwisha, unapata malaria.

¹² Na—na halafu kuna nyoka anayeitwa mamba. Akikuuma, unaishi kama muda wa dakika mbili hivi tu akiisha kukuuma.

¹³ Kisha kuna swila wa manjano. Unaishi kama dakika kumi na tano akiisha kukuuma. Na mmoja wao alikuwa karibu sana na mwanangu, kiasi cha yeye kuweza kumgusa kichwani. Tayari ameisha simamimisha kichwa, amuume, kabla hatujampiga risasi, hali kama hiyo.

¹⁴ Kisha kuna swila mweusi. Loo, kuna kila kitu tu! Na halafu hatari za wanyama mwitu, bila shaka, simba, simba marara, ama chui, na kila kitu cha kukabiliana nacho, huko mwituni. Halafu magonjwa, kuna kila namna ya magonjwa kule.

¹⁵ Nawe una hayo yote ya kukabiliana nayo unapoenda. Mbali na hayo, tena kuna wachawi kukusai kila mahali, unaona, na ushirikina wao wote na kadhalika. Lakini, jinsi gani, ni jambo la ajabu jinsi gani kumwona Bwana wetu akiyaondolea mbali, kila upande, namna hiyo, ndipo unaendelea.

Na siku hiyo ninakumbuka, nikiwa nimesimama, vizuri sana, yale yaliyotukia, nitawaambia wakati fulani katika mkutano mwingine, maana nataka kufikia somo langu alasiri ya leo, la *Elimu Juu ya Pepo*.

¹⁶ Lakini sasa, na jambo hili nilikuwa nikiliwazia, nilipokuwa nimeketi pale, mwisho utakuwa ni nini? Na niliporudi kutoka nchi za ng’ambo, ninajua tulikuwa na kama watu laki moja walioongoka tulipokuwa kule. Na mzee Ndugu Bosworth akaja kwangu. Kasema, nikasema, “Vema, Ndugu Bosworth?”

¹⁷ Akasema, “Naona fahari sana juu yako, Ndugu Branham!” Akasema, “Ndio kwanza—ndio kwanza unayaanza maisha,” basi akasema.

¹⁸ Nikasema, “Vema, nafikiri yamekwisha.” Nikasema, “Mimi nina umri wa miaka arobaini na. Nafikiri nilipiga vita vizuri na kumaliza mwendo.”

¹⁹ Akasema, “Umepita umri wa miaka arobaini?” Kasema, “Nilikuwa na umri huo kabla sijaongoka.” Kasema, “Ningali ninasonga mbele vizuri.” Alikuwa anakaribia sana kwenye mwaka wake wa themanini. Na ninii tu. . .

Nikawaza, “Vema, labda kwa namna fulani hiyo ni kweli.”

²⁰ Kwa hiyo akasema, “La, wewe ni Branham mpya kabisa sasa. Unajua tu namna ya kuendeleza mikutano yako vizuri zaidi, na kila kitu.” Kasema, “Ukipata tu kuishika Marekani kwa njia nzuri, ukiwa na mkutano uliopangwa vizuri, ambapo unaweza kukaa majuma sita ama nane katika mahali fulani, na kuuandaa na kuutangaza kila mahali,” kasema, “utafanya jambo, lakini, na kwa ajili ya Bwana wetu.” Kwa hiyo tukaendelea, tukaendelea namna hiyo tu, kwa hiyo yalikuwa ni matamu sana—matamu sana.

²¹ Ndipo baada ya muda kidogo, nikaona ono, wakati nilipokuwa Marekani, nalo likatimia, na likanirudisha Afrika, na likanionyesha mkutano ule ule, tukiketi kule mbele ya Durban. Na mkutano wa kwanza ukaishia katika historia, kwenda kuelekea Magharibi. Mkutano wa pili ukaja na, wakati ulipokuja, ulikuwa bado mkubwa kuliko mkutano wa kwanza ulivyokuwa. Naye. . . Nikasikia kiyowe, na Malaika alikuwa akishuka kutoka Mbinguni; Alikuwa na mwanga mkuu.

²² Na yule Malaika wa Bwana anayesimama karibu nasi hapa, alikuwa amesimama, daima anasimama upande wangu wa kuume, kwa upande huu. Naye alikuwa amesimama pale, na alikuwa—alikuwa akizunguka. Nami nilimwona Mtu huyu amesimama chini Yake. Yeye—Yeye si-. . . Sasa, hilo si ono unapomwona Yeye. Ni halisi tu kama unavyoniangalia. Mbona, unaweza kumsikia akitembea na kuzungumza nawe. Na wakati Yeye. . . Jambo lo lote, ni halisi tu. Wala si ono; Mtu huyo amesimama tu pale kama tu unavyosimama wewe. Na sauti Yake ni kama tu ambavyo ya kwangu ingekuwa ama yako ingekuwa. Lakini ono, ni jambo ambalo linatokea mbele yako na unaliona, namna hiyo. Lakini Mtu huyu anakuja tu na kusimama pale.

²³ Kwa hiyo aliniambia yale yatakayotendeka. Naye akasema ya kwamba. . . Malaika huyu akashuka, Naye akaniambia nigeuke niangalie upande *huu*. Na ilionekana ni kuelekea India, sasa. Sisemi ni India, lakini ni karibu. Lakini walikuwa ni Wahindi.

²⁴ Maana, Waafrika ni wakubwa, wenye maungo, watu wanene na wazito hivi. Wengine wao wana urefu wa karibu futi saba, na uzito, loo, ratili mia mbili themanini, mia tatu, wenye maungo. Wazulu, sasa, Washanghai na Wabasuto, nao loo, kuna makabila mengi mbalimbali. Kulikuweco na makabila kumi na matano yaliyoketi pale siku ile, niliyokuwa nikizungumza nao.

25 Ningesema neno moja, kama vile, “Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.” Ningeenda ninywe maji kabla halijapitia kwa wakalimani wote. Mmoja angesema . . . Na kelele hizo zote!

Nilikuwa nikifikiri, nilipowasikia Wapentekoste wakinena kwa lugha, ya kwamba labda mmoja ananena katika aina moja ya sauti na mwingine nyingine, hiyo ingewezekanaje duninani? Lakini ninaamini Biblia ni kweli, na ninajua ni kweli, wakati iliposema, “Hakuna sauti isiyo na maana.”

Wengine wao wangesema, mmoja wao aseme, “Bliri bliri bliri bliri,” hayo yalimaanisha “Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.” Mwingine angesema, “Klaki klaki klaki klaki,” hayo yalikuwa ni “Yesu Kristo, Mwana wa Mungu,” katika lugha yake. Kwa hiyo haidhuru ni sauti ya namna gani, ina maana mahali fulani. Hiyo ni kweli. Haidhuru ni sauti ya namna gani, inamaanisha jambo fulani kwa mtu fulani mahali fulani. Na wakati Yeye alipo- . . . Walitoa hilo.

26 Ndipo nikaona kwamba kwenye mkono wangu wa kushoto, yule Malaika aliposhuka akaja na nikaona kitu kama umati mkubwa pale, nao walikwa watu wenye . . . walionekana kama walikuwa wamejizungushia le—leso, namna *hii*, na walikuwa wamejizungushia na kuifunga, kama vile kumzungushia mtoto mchanga, nepi. Na ilikuwa hivyo. Nami ningeweza kuona umbali nilioweza kuona, hakuna cho chote ila watu tu. Na kisha Malaika huyu akawasha taa kubwa iliyobembea, na ikaanza kubembea kwenda mbele na nyuma, namna *hiyo*. Nami sijawahi kuona watu wengi namna hiyo maishani mwangu!

27 Na halafu Malaika huyu mwingine akaja karibu yangu kabisa, na kusema, “Wako watu laki tatu katika mkutano ule.” Nami nimeliandika hapa. Nanyi liandikeni katika namna fulani ya kipande cha karatasi, kama nilivyowaambia juu ya yule mvulana mdogo akifufuliwa kule Finland. Andikeni hilo kwenye ukurasa wa kwanza wa Biblia zenu mahali fulani, ya kwamba katika mkutano huu (Kutakuweko na mkutano. Nanyi mtasikia habari zake kwa njia fulani.) wa watu laki tatu watakaohudhuria mkutano huo. Sasa, angalieni kama hilo si kweli. Huo utakuwa mkubwa mara tatu ya ulivyokuwa ule mwingine. Mnaona? Watu laki tatu watakaohudhuria mkutano huo. Nami ninafurahi sana kupata kwenda kule, sijui nifanyeje, kwa maana mimi napenda kuwavuta watu kwa Bwana.

28 Na pale, wakati mmoja, niliona—niliona wapagani kweli kweli elfu thelathini wakija kwa Yesu Kristo katika wito mmoja wa madhabahuni, wapagani kweli kweli elfu thelathini.

29 Sasa hebu na twende kwenye somo letu upesi sana. Jana tulijifunza mbinu za pepo. Nimekuwa nikiwazia leo, ninavyoongozwa na Mungu. Hamjui ni uhuru jinsi gani kutoka. Sasa, mimi si mwalimu. Mimi niko mbali sana na kuwa mwa—mwalimu wa Biblia. Nami ni . . . Elimu yangu imeishia darasa

la saba. Kwa hiyo hiyo ni. . . Na, hiyo, nilitoka shuleni yapata miaka ishirini na mitano iliyopita, kwa hiyo huo ni wakati mrefu sana. Nami sina elimu nyingi, lakini yote ni juu ya ni yale ninayopata kwa uvuvio. Na kama uvuvio huo hauulingani na Biblia, basi si wa kweli. Unaona? Hauna budi kuwa ni Biblia. Hata uwe ni uvuvio wa namna gani, hauna budi kuja. . . *Huu* hapa ndio msingi wa Mungu. Hakuna msingi mwingine uliowekwa ila *Huu*. Na kile *Huu* ulicho, kama yale ambayo ningesema yangukuwa kinyume cha Hili, acheni maneno yangu yawe uongo, kwa maana Hili ni Kweli. Unaona? Unaona? Na kama malaika fulani angewaambia jambo fulani ambalo lingekuwa tofauti na Hili, Paulo alisema, “Na awe laana kwenu,” yaani hata malaika wa Nuru. Sasa, kuna mambo mengi makuu. Mimi nilininii tu. . . ninii tu. . . Nilichagua siku mbili, ili niwaletee watu somo hili, hizo zilikuwa jana na leo, kwa ajili ya mikutano ya alasiri.

³⁰ Sasa, sababu ya mimi kufanya jambo hili, ni kujipa mwenyewe jaribio dogo kuona kama Mungu angenisaidia. Kuna jambo fulani moyoni mwangu. Na hili ni, ya kwamba, baada ya Ujumbe huu mkuu, na baada ya Mungu Mwenyewe kuthibitisha yale ambayo nimesema kwamba ni Kweli, katika Neno Lake; kwa Neno Lake, kwanza, halafu kwa ishara na maajabu. Sasa, ninafikiri, kwa Kweli ya Injili kwa Kanisa, mimi ninawajibika, kwa Mungu, kuleta jambo hili kwa Kanisa. Hiyo ni kweli. Wao wamegawanyika sana, katika madhehebu mengi sana, na vikundi vyake vilivyojitenga, hata jambo hilo ni kosa. Sisi sote ni watoto wa Mungu tunapozaliwa mara ya pili, Hivyo, unaona. Na ukweli wa mambo ni kwamba Mungu anatutaka tujue jambo hilo, ya kwamba sisi ni watoto Wake.

³¹ Sasa, kumbukeni, lile hekalu la Sulemani lilikuwa limekatwa, kutoka kila mahali ulimwenguni. Na hapa jiwe likaja limechongwa *hivi*, na jiwe moja limechongwa *vile*, na jiwe moja limechongwa *hivi*, na lingine limechongwa *vile*, lakini, yalipowekwa pamoja, hapakuwepo na mlio wa msumeno, wala sauti ya nyundo, kila kitu kilienda moja kwa moja mahali pake. Mungu alikuwa ndiye Fundi wake.

³² Mungu ana kanisa linaloitwa Assemblies, na moja linaloitwa kanisa la Mungu, na moja liitwalo *hivi*, na lingine *vile*. Na, lakini wakati yote yatakapokusanyika pamoja, litakuwa ni kundi moja kuu la upendano wa ndugu, naye Mungu ataweka, atalikusanya Kanisa hilo pamoja na kulinyakua mbinguni.

³³ Kila picha inayojulikana sana, kabla haijawekwa kwenye ukumbi wa sanaa, haina budi kutundikwa, kupitishwa kwenye ukumbi wa wakosoaji, kwanza. Yule mtu aliyechora, pupa. Ama, samahani, siwezi kukumbuka jina lake, alichora Meza ya Bwana Ya Mwisho, hata hivyo, ilimchukua maisha yake yote. Aliichora picha hiyo. Ilichukua muda wa kama miaka ishirini, ama miaka kumi, ninaamini, kati ya kumchora Kristo

na Yuda. Na je! mlijua, katika picha hiyo mashuhuri, ya kwamba mtu yule yule aliyejitoa achorwe Kristo, miaka kumi baadaye alijitoa achorwe Yuda? Hiyo ni kweli. Alichorwa. Miaka kumi ya dhambi, kutoka mwimbaji mashuhuri wa taarabu, kupachukua mahali pa Kristo, akaja mahali pa Yuda. Haikulazimu kuchukua miaka kumi. Inachukua dakika kumi, itakufanyia jambo lile lile. Itabadilisha tabia yako, katika dhambi. Lakini, hata hivyo, picha hiyo ilipitia kwa wakosoaji wote.

³⁴ Na jambo hilo ndilo ninalofikiria kuhusu Kanisa la Mungu, kundi ambalo limeitwa. Vema, sisemi jambo hili kwa kuwalaumu. Nimeabiri bahari saba, nami niko kwenye safari yangu ya tatu kuzunguka ulimwengu, na watu wanasema, “Mtakatifu anayejifingirisha! Mtakatifu anayejifingirisha!” Nami nimetafuta ulimwengu mzima, nami sijapata kuona mtakatifu anayejifingirisha bado. Hilo ni jina ambalo Ibilisi amewabandika watu. Hivyo tu. Hakuna kitu kama mtakatifu anayejifingirisha. Nami nina takwimu za kila makanisa mia sita na sitini na manane yaliyopo, na yaliyounda madhehebu ulimwenguni, hakuna hata moja ya hayo linaloitwa Mtakatifu Anayejifingirisha. Na hiyo ni kutoka serikalini. Hakuna kanisa moja la Mtakatifu Anayejifingirisha nilijualo. Kwa hiyo, kilikuwa ni kitu fulani tu Ibilisi alichokipa jina. Lakini, sasa, katika haya yote, mambo haya yote, Mungu ameichora picha. Na wakati mmoja maskini makanisa haya madogo yaliyokuwa hapaa, baadhi yenu. . .

³⁵ Ninawaangalia watu hawa wenye mvi. Kijana wangu wa kiume, jana; nilikuwa chumbani, ninasoma, na mhudumu mmoja akaja na kusema, “Ningetaka kupeana mkono na baba yako.” Bila shaka, kijana wangu amelelewa na Ndugu Baxter na hao wengine, ambao wananinii tu, “La,” ndio hivyo, upesi. Sipendi jambo hilo. Mnaona? Haidhuru kama mimi. . . Bila shaka, siwezi kuwa mtumishi wa mwanadamu na wa Mungu, pia. Lakini nadhani mimi napenda kupeana mikono na ndugu zangu. Ninapenda kufanya jambo hilo. Kuna kitu fulani katika jambo hilo, ninapenda kupeana mikono na—na mhudumu. Si mhudumu tu, lakini mtoto ye yote wa Mungu, ninapenda kufanya jambo hilo. Sikuwa na habari mpaka mke wangu aliponiambia baadaye kidogo. Vema, kama angeweza kumwambia mhudumu huyo, “Hebu kidogo, yeye yuko kule katika maombi, na—nami nitaona atasemaje.” Vema, hilo, hilo lingekuwa afadhali. Kwa hiyo nikamsahihisha kidogo juu ya jambo hilo, asifanye hivyo. Unaona?

³⁶ Na kwa hiyo ni kweli, huwezi tu kushughulikia mambo yote, kama alivyosema yule ndugu muda kidogo uliopita. Kama ukifanya namna hiyo, basi usiku ni—nimechoka sana, mnaona. Watu wanaanza kuzungumza, na kila mmoja labda ana ugonjwa, na wanapokuja kuzungumza juu yake, upesi, Malaika wa Bwana anatokea papo hapo kunena habari za mtu huyo.

³⁷ Kuna mtu fulani anayeketi hapa, anayeniangalia moja kwa moja sasa, anayejua kwamba jambo hilo ni kweli, tangu dakika chache zilizopita, ama kama saa moja na nusu iliyopita. Mama fulani anayeketi hapa, ambaye hakujua ilikuwa ni kitu gani, ambapo Malaika wa Bwana alinena naye hivi majuzi usiku na kumwambia jambo fulani, naye hakuweza kulipata jambo hilo. Lakini leo limetukia, kwa hiyo yeye anajua sasa maana yake wakati Yeye alipokuwa akizungumza naye. Na ambavyo, akiwa amesimama pale akinena naye, Malaika wa Bwana alirudi moja kwa moja na kumwambia shida yake ilikuwa ni nini, na habari zake zote, na—na yale aliyokuwa akiwazia, na mmoja wa wapendwa wake, na vile Mungu alivyonena na kusema ya kwamba alikuwa amethibitisha jambo hilo, na yale ambayo yangetukia. Kwa hiyo hivyo ndivyo litakavyokuwa hasa. Mnaona? Mungu alikuwa amesema jambo hilo.

³⁸ Vema, sasa, vipi mara zile chache ambazo daima . . . Halafu, kila ono linakudhoofisha kiasi hicho zaidi, unaona. Na muda si muda unajua, unapofika kanisani usiku, umechoka tu kabisa hata ni vigumu kujua la kufanya. Nanyi niombeeni sasa, mnaona, kwa sababu ni kutoka kwenye mkutano mmoja kwenda mwingine, kwenda mwingine. Kama ungalikuwa ni mkutano huu tu, ingekuwa ni tofauti, kama ningalikuwa ninaenda nyumbani hivi sasa wala nisiende kufanya lo lote kwa miezi kadha, ningaliondoka niende nichukue ndoano yangu niende nikavue samaki. Lakini sina budi kwenda kutoka kwenye mkutano mmoja hadi mwingine moja kwa moja, kutoka mmoja hadi mwingine, mnaona. Hilo ndilo linalosababisha jambo hilo.

³⁹ Nanyi nyote muombe, ninyi watu huku nyuma kwa wasikilizaji. Waliniambia jana usiku ya kwamba . . . [Mahali patupu kwenye kanda—Mh.] . . . hawakuitikia ule wito. Sasa, hiyo ni hatari sana, mnaona. Wakati waliposema jambo hilo . . . Vema, wakati mwingine taa hizi hazitoi nuru, kuna mahali penye giza pale katikati.

⁴⁰ Nami ninamwangalia Malaika wa Bwana wakati anaposimama hapa, ninaweza kumhisi. Halafu nitamsikia akiondoka kwangu, nami nitaangalia, ataondoka kwangu na aende mahali fulani na kusimama pale kidogo, nami naweza kumwona. Ndipo atamulika na ono litatokea. Ndipo nitaona hilo ono. Nitaangalia ni mtu wa namna gani ambaye yeye yuko karibu naye pale. Ninamwona mtu huyo, ndipo nitanena. Hilo ndilo linalotukia. Hivyo ndivyo inavyotendeka. Si lazima umwambie kila mtu jambo hilo, lakini hilo—hilo ndilo linalotendeka, mnaona. Yote yako kwenye ulimwengu wa kiroho.

⁴¹ Ndipo kama mtu huyo hajibu kitu, itakuwa ni kama kusoma Biblia hapa na kusema, “Hayo yote ni bure,” anaiacha. Mnaona? Kwa hiyo hilo linakuwa ni baya sana. Kwa hiyo iweni macho,

mwe mnasikiliza, mwangalie. Akinena, jibu. Unaona, iweni tayari tu kujibu wakati wo wote.

⁴² Na kwa hiyo mke wangu, na Ndugu Beeler na wengine wengi, asubuhi ya leo, walikuwa wakiniambia habari hizo, ya kwamba ilikuwa inamwitwa mwanamume fulani juu ya ndugu yake, mahali fulani, ambaye alikuwa na shida fulani, na kadhalika. Na mtu huyo hakuitikia huo mwito, kwa hiyo huwezi kulizua jambo hilo. Hiyo ni kati ya Mungu na mtu huyo. Ono liliniacha. Ndipo sikuweza kulipata tena, kwa sababu yeye hakujibu. Kwa hiyo, mwe waangalifu, mwe macho.

⁴³ Sasa nikitukua somo hili la *Elimu Juu ya Pepo* na kuzungumzia juu ya pepo. Sasa, watu, wakati mtu unaposema “pepo,” upesi sana watu wanaanza kufikiria, “Loo, mshupavu wa dini ama cho chote kile!” Lakini pepo ni halisi tu kama ilivyo Malaika. Ni halisi kabisa.

⁴⁴ Na Ibilisi ni pepo halisi tu, kama vile Yesu Kristo alivyo Mwana wa Mungu. Yeye ni pepo! Mbingu ni halisi vile vile tu. Na kama hakuna kitu kama kuzimu, hakuna kitu kama Mbinguni. Na kama hakuna Milele iliyobarikiwa... Hukumu ya Milele, hasa, hakuna Milele iliyobarikiwa. Kama hakuna mchana, hakuna usiku. Mnaona? Lakini hakika tu kama vile kulivyo na mchana, kuna usiku. Ha—hakika kadiri kulivyo—kulivyo na Mkristo, hapana budi kuwe na mnafiki. Hakika kadiri kulivyo na mtu aliye halisi anayetoka kwa Mungu, kuna mtu fulani wa kumwiga mtu huyo. Mnaona? Ni kitu halisi tu na kinyume, cheusi na cheupe, moja kwa moja katika maisha na kila kitu, kweli na uongo kila mahali. Na kuna injili ya uongo, kuna Injili ya kweli. Kuna Ubatizo wa kweli, kuna ubatizo wa uongo. Kuna kiinimacho, na kuna cha kweli. Kuna dola ya kweli ya Kimarekani, na kuna dola bandia ya Kimarekani. Kuna Mkristo halisi, kuna mnafiki halisi, unaona, hiyo ni kuiga tu. Kwa hiyo unaona ya kwamba, kwa hiyo yote yanaambatana pamoja. Sasa, hatuwezi kuitenganisha. Mungu huifanya mvua kunyesha.

⁴⁵ Na anijalie kuzungumza hapa kidogo tu. Ni wahubiri wangapi waliopo hapa, inueni mikono yenu. Kila mahali, wahubiri, hebu tuone mikono yenu. Vema, Mungu awabariki, ndugu. Sasa, sasa, usichukue jambo hili kama fundisho sasa, lakini, kabla tu hatujalikaribia somo hili muhimu sana, nitawaambia nini. Ni Wapentekoste wangapi waliopo hapa? Inueni mikono yenu pote, kila mahali. Vema, nyote ni Wapentekoste. Vema. Nitawaambia nilichopata nilipoingia kwenye makusanyiko yenu, kundi.

Nilikuwa papa hapa Indiana, mahali pamoja panapoitwa Mishawaka. Kundi la kwanza la Wapentekoste nililopata kuona, walikuwa wanaitwa Pe—Pentekote Assemblies ya Yesu Kristo, naamini, ama kitu kama hicho, kundi zuri sana la watu. Sasa limeunda madhehebu na wanajiita United Pentekoste.

Walitengana na hao wengine, kwa sababu ya hoja ya ubatizo wa maji. Hilo haliwafanyi wanafiki hata kidogo. Kuna Wakristo wengi halisi, waliozaliwa mara ya pili, waliobatizwa na Roho Mtakatifu katika makundi yao. Na Mungu aliwapa ubatizo wa Roho Mtakatifu kwa kubatizwa katika “Jina la Yesu,” na kuwapa wengine ubatizo wa Roho Mtakatifu, kwa kubatizwa katika “Baba, Mwana, Roho Mtakatifu.” Kwa hiyo, “Mungu huwapa Roho Mtakatifu, wale wanaomtii,” kwa hiyo ni nani—ni nani waliopata, nani waliomtii Yeye? Hilo hapo.

⁴⁶ Kama mkisahau tu, na hao wanaotaka kuwa hivyo, acha wawe, nanyi mwendelee kuwa ndugu. Hivyo tu. Msininii. . . Kile kilichosababisha jambo hilo, kilikuwa ni kule kutengana kwao, kutengana. Mnaona? Nini? Ilikuwa ni kutengana, kugawanyika, kutenganisha undugu, kuondoka na kujitenga. La, bwana, sisi hatujagawanyika, sisi ni mmoja. Hiyo ni kweli.

⁴⁷ Lakini nilipokuwa nimesimama pale, nilikuwa nikiwaangalia watu hao. Sasa, mimi, nilitoka tu kutoka kwenye kanisa la kawaida la Kibatisti la Kusini, mbona, nilikuwa nimewaona watu hao, nililingia kule nao walikuwa wakipiga makofi, wakishangilia, “Mmoja wao, Mmoja wao, nafurahi kusema mimi ni mmoja wao!”

⁴⁸ Nikawaza, “Jamani! Whiu! Muda si muda, huyu hapa anakuja mtu fulani akapitia pale, anacheza kwa nguvu awezavyo. “Tu-tu-tu-tu-tu,” nikawaza, “ni desturi gani hizi za kanisa! Sijawahi kusikia vitu kama hivyo.” Nikaendelea kuwaangalia, kila upande. Nikashangaa, “Vema, hawa watu wana nini?”

⁴⁹ Sasa, mlinisikia nikisimulia hadithi ya maisha yangu, mahali nilipofika kwenye mkutano ule pale. Lakini hili ni jambo moja ambalo sijawahi kusimulia, sijawahi kulisimulia hapo kabla, hadharani. Kwa hiyo wao. . . Sasa, kama unataka kuyafuta kwenye kanda yako, mbona, unaweza kufanya jambo hilo. Vema. Sasa, katika jambo hili niliangalia, na sasa nikawazia, “Vema, hao watu ndio watu wenye furaha kuliko wote niliowahi kuona maishani mwangu.” Hawakuionea aibu dini yao. Sisi Wabatisti huona haya kidogo tu, mara kwa mara, mwajua. Mnaona? Na walipoingia katika maombi, unajua, wanarudi nyuma ya pepeo, unajua. Na—na, lakini sisi. . . Lakini hao watu hawakuwa, ndugu, wao—wao walijaa dini ndani kote, nje, na kila mahali miilini mwao.

⁵⁰ Vema, ninakumbuka usiku ule wakati nilipoenda mimbarani. Kasema, “Wahubiri wote waje jukwaani.” Ulikuwa ni mkutano kwa mtu ye yote. Iliwabidi waufanyie hapa Kaskazini, kwa sababu ya—kwa sababu ya matatizo ya ubaguzi wa rangi, ile sheria ya Jim Crow ya Kusini. Kwa hiyo wote walikutana pale kutoka kila mahali. Kwa hiyo, nilikuwa nimeketi pale. Naye akasema. . . Vema, sasa kuna. . .

Nikawasikiliza wahubiri wote siku hiyo nzima na usiku huo. Wakasema maskini mhubiri mmoja mzee, ilikuwa mzee mmoja mweusi aliyetoka, na mzingo mdogo wa nywele kuzunguka kichwa chake, namna *hiyo*, amevaa koti kubwa lenye mkia la wahubiri, unajua, ukosi wa mahameli, na kulikuwa ni joto. Maskini mzee huyo alitokea pale namna *hii*. Akasema, “Watoto wangu wapendwa,” akasema, “Nataka kuwaambieni,” akaanza kutoa ushuhuda. Niliikuwa karibu ndiye mwenye umri mdogo sana kwa wale tuliokuwa tumeketi jukwaani. Kwa hiyo basi akasema, “Nawaambia!” Alichukua somo lake kutoka kwa Ayubu, “Ulikuwa wapi lilipoiweka misingi ya nchi? Niambie ilikazwa juu ya nini.”

⁵¹ Wahubiri hawa wengine wote walikuwa wamehubiri juu ya Kristo, yale mambo ya kawaida. Niliwasikiliza, nikawafurahia. Lakini si huyu mzee kijana! Yeye alirudi huko nyuma kama miaka elfu kumi kabla ulimwengu haujaanza. Akapaa Mbinguni kisha akashuka chini kuvuka anga, yale yaliyokuwa yakitukia. Yale waliyokuwa wakihubiri, akiendelea, wakati wa mchana; alikuwa akihubiri juu ya yale yaliyokuwa yakitendeka Mbinguni. Akamrudisha Kristo katika upinde wa mvua uliolala, akarudi kule nyuma mahali fulani katika Umilele. Mbona, hakuwa amehubiri dakika tano hivi hata maskini mzee huyo, Kitu fulani kikamwingia. Akaruka juu hewani na kugonganisha miguu yake pamoja, na ku sema kwa sauti kuu, “Hoyee!” Alikuwa na nafasi kubwa kama niliyo nayo hapa. Akasema, “Hamna nafasi ya kutosha kwangu kuhubiri,” na huyoo akaondoka.

⁵² Vema, nikawaza, “Kama hicho kitamfanya hivyo mtu mwenye umri wa karibu miaka themanini, kingenifanya nini mimi? Hicho ndicho ninachotaka.” Hicho ndicho ninachotaka.

⁵³ Lakini kilichonipata kilikuwa ni hiki. Sasa, tunazungumza juu ya pepo sasa. Kilichonipata, niliwaangalia wanaume wawili. Mmoja aliketi upande mmoja, na mwingine ule mwingine. Na wakati Roho alipoanguka, hao watu wangeinuka na kunena kwa lugha na kupaza sauti, na midomo kubadilika kuwa myeupe. Ndipo nikawaza, “Loo, jamani, laiti ningalipata kitu hicho!” Mnaona? “Ni ajabu vipi! Loo, hilo ni ninii . . . Ninapenda tu jambo hilo!” Vema, nilitoka nikaenda kwenye shamba la mahindi. Nami niliwahadithia hadithi ya maisha yangu. Mliisoma kwenye kile kitabu. Nikalala usiku kucha. Ndipo nikarudi asubuhi yake, kwa hiyo nikawazia ningejaribu tu. Nina njia ya kufanya mambo ambayo hakuna aijuaye ila mimi na Mungu. Kwa hiyo, hilo, ninachukua mfano na ninaenda kukutana na roho ya mtu huyo. Mmeona jambo hilo papa hapa jukwaani. Mnaona? Na kwa hiyo basi nikaanza kuzungumza na mmoja wa watu hao. Niliwaona, waliketi karibu, nao wangeshikana mikono tu na kucheza na kupaza sauti. Nikawaza, “Loo, jamani, hilo linasikika halisi kwangu!”

54 Ndipo nikashika mmoja wa mikono yake. Nikasema, “U hali gani, bwana?”

55 Akasema, “Sijambo.” Mtu mzuri sana, muungwana. Akasema...

Nikasema, “Je! wewe ni mhudumu?”

Akasema, “La, Bwana. Mimi ni mfuasi wa kawaida tu.”

56 Ndipo nikaendeleza mazungumzo pamoja naye kusudi niipate roho yake. Unaona? Yeye hakujua hilo. Hakuna mtu aliyejua. Sikusema lo lote juu ya hilo. Miaka kadha baadaye, kabla sijalitaja jambo hilo. Kwa hiyo wao... Lakini nilipokuja kutambua, ilionekana ni kweli, kikamilifu kabisa, mwanamume Mkristo halisi! Mtu yule alikuwa mtakatifu wa Mungu kabisa. Nikawazia, “Ndugu, hilo ni sawa.”

57 Lakini upande ulioshangaza, nilipompata huyo mtu mwingine, ilikuwa ni kinyume. Alikuwa hata anaishi na mwanamke ambaye hakuwa mkewe. Hiyo ni kweli. Nami nikaona limemwelekea, lile ono. Nikawaza, “Loo, jamani, haiwezekani.” Na mtu huyo... Nikawazia, “Hebu, hebu, roho hii iliyo kati ya watu hawa ni mbaya. Hakuna la zaidi.”

58 Kwa hiyo usiku huo wakati ninii... nikahudhuria mkutano, na zile baraka zilikuwa zikishuka, ningemwomba Mungu, na Roho Mtakatifu, Malaika wa Bwana akashuhudia ya kwamba ilikuwa ni Roho Mtakatifu. Na Roho yule yule aliyekuwa akishuka juu ya mtu *huyu* alikuwa anashuka juu ya mtu *yule*. Na wakati Roho aliposhuka, wote wawili wangeinuka, na wote wawili wanapaza sauti na kupiga makelele na kumsifu Bwana, na kunena kwa lugha na kucheza. Nikasema, “Si—si—siwezi hata siwezi kuelewa, Bwana. Ile... Siwezi kuliona katika Biblia, ambapo jambo hilo lingekuwa sahihi.” Sasa nikasema, “Labda nimedanganyika.” Unaona? Nikasema... Sasa, hapa, si—siwezi... Mi—mimi ni wa kimsingi kabisa katika Biblia. Hapana budi iwe ni Hii. Mnaona? Nikasema, “Bwana, unajua hali yangu, na si—sina budi kuliona katika Neno Lako. Na—nami siwezi kuelewa. Wakati Roho Mtakatifu anaposhuka juu ya mtu *huyu*, Roho Mtakatifu anashuka juu ya mtu *yule*, na mmoja wao ni mtakatifu na huyo mwingine ni mnafiki. Nami ninajua ndivyo ilivyo.” Ninajua jambo hilo. Bila... Ningeweza kumchukua huyo mtu nje na kumthibitishia, ama kumwita papo hapo na kumwambia juu ya jambo hilo.

59 Kama vile ningeweza kufanya kwa mtu yule aliyekuwa ameketi papa hapa jana usiku, hakuwa kitu ila mwi—mwigaji, kama kulipata kuwepo na mmoja ameketi pale. Nami ilinipasa kumfichua, lakini angaliinuka na kuanza kufanya fujo. Kwa hiyo nikaliachilia tu, kwa ajili ya mkutano huo, lakini nilimjua. Naam, bwana.

Kuna mmoja, wawili wao, walioketi nyuma kule kabisa, juzi usiku, wafuasi wa kanisa fulani papa hapa mjini.

Wabishi kwelikweli! Niliwaona. Lakini, kama ukifanya jambo hilo, linasababisha matatizo. Nimefanya jambo hilo mara nyingi. Ninawaacha tu. Ni sawa. Mungu anajua, Yeye ndiye Hakimu. Hebu waniite wakati mmoja, na ndipo mtaona kitu kitakachotukia, mnaona, hebu na wajibu.

Kama yule pepo, sikumtoa huyo pepo. Yeye alinjia tu na kunisai. Hapo ndipo Mungu alipoingia kutenda kazi, unaona, hiyo ni kweli, nanyi mliona kilichotukia. Vema. Lakini ninayaachilia tu. Ingeufanya mkutano kuwa mgumu, kwa maana huyo roho alikuwa anafanya kazi ndani yangu, unaona. Na kwa hiyo niliendelea tu.

⁶⁰ Lakini sasa, hawa watu, sikuweza kuelewa na jambo hilo. Na ilikuwa ni miaka miwili baadaye, ama mitatu, nilipokwenda kule Green's Mill, Indiana, hapa, kwenye kambi ya maskauti. Nilikuwa nimerudi kwenye pango la kale ambamo mimi huenda kuomba. Na kule nyuma, nikasema, "Bwana, siwezi kufahamu kilicholipata lile kundi la watu. Watu wazuri sana niliowahi kukutana nao maishani mwangu, na—nami siwezi kuelewa jinsi hiyo inavyoweza kuwa roho mchafu. Wakati ni ninii... iwapo basi... Wewe unajua unyofu wa moyo wangu. Unajua jinsi ninavyokupenda na jinsi nilivyokutumikia. Na Roho yule yule aliye hapa, pamoja nami, alikuwa kwa na hao watu. Na hapa Huyu alikuwa juu ya jamaa yule, pale, vile vile tu." Kwa hiyo sikuweza kuelewa.

⁶¹ Ndipo Bwana akashuka katika rehema Zake na kunionyesha. Jambo lenyewe lilikuwa ndilo hili hapa. Halina budi kuwa ni la Kimaandiko, kwanza. Yeye akasema, "Chukua Biblia yako." Ndipo nikaichukua Biblia yangu. Nakisia niliishikilia Biblia hiyo kwa dakika kumi bila mtu ye yote... Neno lo lote kuja. Nilingojea tu kwa dakika chache. Nikamsikia akisema tena, "Fungua Waebrania 6 na uanze kusoma." Nami nikafanya hivyo. Na wakati ilipofikia pale chini, ambapo ilisema, "Mvua huja juu ya nchi kuitia maji mara kwa mara, na kuzaa mboga zenye manufaa... bali ikitoa miiba na michongoma, hukataliwa, ambayo mwisho wake ni kuteketezwa." Nami nikalipata papo hapo.

Nikawazia, "Hilo hapo. Mungu ashukuriwe! Hilo hapo." Unaona?

⁶² Sasa, Yesu alisema, "Mpanzi alitoka akaenda kupanda mbegu," sivyo? Sasa, ninyi nyote mu Wakristo hapa. Kila mtu aliinua mkono wake, hata hivyo, Wapentekoste, Wakristo waliozaliwa mara ya pili. Vema. Wao... Naye alisema, "Mpanzi alitoka akaenda, akipanda mbegu. Na wakati alipolala..." Kupumzika kwake, mauti, katikati. Unaona? "Na wakati alipolala, adui alikuja akapanda magugu katika shamba lile." Magugu ni nini? Makwekwe, miiba na kadhalika. Sasa, "Na wakati mwenye shamba (mhubiri) alipoona magugu yakikua,

kasema, ‘Hebu niende nikayang’oe.’ Yeye akasema, ‘La, la. Utang’oa na ngano pia. Viache vyote vikue pamoja.’”

⁶³ Kuna shamba la ngano kule. Kuna mimea itambaayo, kiwawi, magugu yenye harufu mbaya, kila takataka mle ndani. Hiyo ni kweli? Lakini, sasa, mle ndani mna ngano. Sasa, mvua huja mara kwa mara juu ya nchi, kuinyeshea. Sasa, mvua ni ya nini? Si kunyeshea kiwawi. Sasa angalieni na mwe makini. Si kunyea mtambaazi. Mvua inatumwa kwa ajili ya ngano, lakini kiwawi na makwekwe huona kiu tu kama ngano inavyoona. Na mvua ile ile inayoinyeshea ngano inanyea gugu. Na maskini gugu hilo siku nyingi litasimama wima namna hiyo, nalo likifurahi na kushangilia, vile vile tu kama maskini hiyo ngano ndogo itakavyosimama na kujisimamisha.

⁶⁴ “Lakini kwa matunda yao mtawatambua.” Hilo hapo. Mnaona? Sasa, Roho Mtakatifu yule yule anaweza kumbariki mnafiki. Hilo liliwaangusha baadhi yenu Waarmenia, lakini hiyo ni Kweli. Hiyo ni Kweli. Mmefundishwa utakatifu, ambapo ninaamini katika utakatifu, pia. Lakini Roho yule yule, mvua huwanyea wenye haki na wasio haki, lakini kwa matunda yao mtawatambua.

⁶⁵ Kama nikiangalia huku nje na niende kuchukua ngano, nachukua ngano, lakini magugu yameizunguka. Nayo yanaishi kwa mvua ile ile iliyoinyea ngano. Na mvua hiyo haikutumwa kwa ajili ya magugu, ilitumwa kwa ajili ya Ngano. Lakini mvua hiyo ikiwa huko shambani, ngano hiyo ikiwa . . . magugu yakiwa kwenye shamba la ngano, hupata faida ile ile kutokana na mvua ile ile kama hiyo mingine inavyopata. Na mvua ile ile iliyoifanya ngano kuishi, iliyaifanya magugu yaishi.

⁶⁶ Mambo yote katika maumbile ni mfano wa mambo ya kiroho, kama tunavyofundisha. Hiyo hapo, elimu juu ya pepo, pepo wakiiga Ukristo, hata hivyo, yanazo baraka. Hayo si maziwa ya mtindi, ndugu, kama mnaweza kulikubali. Mnaona? Mnaona? Sasa, ni—ni Kweli.

⁶⁷ Kwa hiyo, siokolewi leo kwa sababu ninaweza kupaza sauti. Siokolewi ati kwa sababu ninajisikia kama kwamba nimeokolewa. Nimeokolewa kwa sababu nimetimiza masharti ya Mungu ya Biblia hili. Yesu alisema, “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele, wala hataingia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani.” Ninaamini jambo hilo. Hiyo ni kweli. Na kwa masharti hayo mimi nimeokolewa, kwa sababu Mungu amesema hivyo.

⁶⁸ Kama angeniambia umeokolewa kwa sababu mtu fulani alisema, “Upepo wa nguvu ukienda kasi ulinigusa usoni,” hilo ni jambo zuri sana, lakini ninataka kujua upepo huo wa nguvu uendao kasi ulitoka wapi kabla ya kunigusa usoni, unaona. Sasa, ni maisha ya namna gani utaenda kuishi baada ya upepo

huo wa nguvu uendao kasi kukugusa? Unaona? Unaona, ni kwa matunda yako unatambulikana. Kwa hiyo, pepo wanaweza kutenda kazi mumo humo miongoni mwa Wakristo. Mnaamini hilo? Mwangelie Paulo, Paulo alisema. . .

⁶⁹ Sasa hapa ndipo ambapo wale wa Siku ya Mvua ya Vuli. . . Kama kuna mmoja wenu hapa, mnisamehe kama ninasema jambo lo lote dhidi yenu. Singesema jambo lo lote dhidi yenu zaidi ya ningalisema dhidi ya Waassemblies, ama wo wote wale, Wabatisti, ama ye yote yule. Kweli ndiyo Kweli. Mahali mlipoacha njia, palikuwa ni hapa: mnawafanya watu manabii na kadhalika ambao si manabii. Manabii hawawekewi “mikono” na kutumwa. Manabii wanazaliwa. Mnaona? Katika Biblia, kuna karama ya *unabii*. Hapo ndipo kosa lenu lilipotokea, kati ya kipawa cha unabii na nabii. Kipawa. . .

⁷⁰ “Mungu, kwa sehemu nyingi na njia nyingi alisema zamani na baba zetu katika manabii, katika siku hizi za mwisho katika Mwanawe, Kristo Yesu.” Na Mwili wa Kristo una karama tisa za rohoni zitendazo kazi ndani yake. Na inaweza kuwa juu ya mwanamke *huyu* usiku wa leo, unabii, labda asiupate tena maishani mwake mwote. Unaweza kuwa juu ya mwanamke *huyu* usiku unaofuata. Unaweza kuwa juu ya mtu *huyu* wakati mwingine. Labda juu ya *yule* kule nyuma wakati huo mwingine. Hilo halimfanyi nabii, halimfanyi mtu ye yote nabii. Ni karama ya unabii ndani yako.

⁷¹ Na kabla mtu huyo ama unabii huo kuweza kutolewa kwa kanisa, hauna budi kupambanuliwa mbele ya waamuzi wawili ama watatu wa kiroho. Hiyo ni kweli? Kulingana, sasa, Paulo alisema, “Nyote mnaweza kutoa unabii, kwa zamu.” Kama neno fulani likifunuliwa *huyu*, *yule* na anyamaze. Vema, hilo lingefanya kundi zima ni manabii basi, kulingana na mafundisho ya siku hizi. La, enyi kanisa la Kipentekoste, tumeyavuruga mambo yote. Na hiyo ndiyo sababu Mungu hawezi kuingia, mpaka tutakapolitua jambo hilo na kwenye Biblia. Hiyo ni kweli. Hamna budi kuchukua njia iliyo sahihi. Mtajengaje nyumba bila kuangalia ramani yake? Unaona? Yakubidi uanze sawa.

⁷² Sasa, ndani mle, nabii, hamjamwona mtu ye yote akisimama kamwe mbele ya Isaya, Musa. Mtu mmoja alifanya hivyo, Kora, siku moja, na kujaribu kushindana naye, Naye Mungu akasema, “Jitenge, nitaifungua ardhi.” Nabii huzaliwa. “Karama na wito havi-. . . majuto.” Hizo ni kukusudiwa na Mungu awali, tangu utotoni hadi utu uzima. Kila kitu kilikuwa kikamilifu kabisa, yale hasa yeye aliyosema yalikuwa ni kweli na aliyathibitisha na kuyaweka wazi. Ni Neno la Mungu, linamjia nabii. Lakini karama ya unabii iko kanisani.

⁷³ Sasa mlisema, “Vema, manabii ni Agano la Kale.” Loo, la! Agano Jipya lilikuwa na manabii.

⁷⁴ Agabo alikuwa—alikuwa nabii wa Agano Jipya. Angalia pale roho ya unabii ikishuka na kumwambia Paulo juu ya jambo hilo. Kisha hapa yuaja Agabo kutoka Yerusalemu, akampata Paulo, na kujifunga kwa mshipi wake, akageuka na kusema, “BWANA ASEMA HIVI, mtu aliyejifunga huu atafungwa kwa minyororo atakapofika Yerusalemu.” Agabo, aliyesimama na kusema, kutabiri yale ambayo yangetukia, alikuwa ni nabii, si mtu mwenye karama ya unabii.

⁷⁵ Na karama ya kuponya na karama zote zile, ewe rafiki yangu Mpentekoste, mlilichanganya. Karama zimo kanisani, kwa mtu ye yote kanisani, mtu ye yote ambaye amebatizwa katika ule Mwili. “Kwa Roho mmoja sote tumebatizwa.” Nayo Biblia ilisema . . .

“Vema, nina karama ya uponyaji.”

⁷⁶ Vema, Biblia ilisema, “Ungamanieni dhambi zenu ninyi kwa ninyi, na kuombeana.” Kila mtu amwombe mwingine. Sisi si kundi lililogawanyikana; sisi ni kundi lililoungana, lililokusanyika pamoja. Mnaona?

Sasa, na hivyo ndivyo pepo wanavyofanya kazi wakati mwingine.

⁷⁷ Sasa angalia yale aliyosema Paulo, “Kama mtu akinena kwa lugha na huyu mwingine afasiri, na lo lote alilosema, na lipambanuliwe kabla—kabla halijapokelewa na kanisa.”

⁷⁸ Sasa, haitakuwa ni kunukuu Maandiko, wala kitu fulani kinginecho kama hicho. Mungu harudii-rudii. Lakini itakuwa ni onyo kwa kanisa. Ndipo kama waamuzi wazuri wakisema, “Na tuupokee huo. Vema, ulikuwa ni wa Bwana.” Wa pili aseme, “Tuupokee huo.” Vinywa vya mashahidi wawili ama watatu, kila neno liimarishwe. Ndipo kanisa linaupokea na kwenda kujitayarisha. Kama jambo hilo halitimii, hicho huo ulichosema, basi mna roho mchafu kati yenu. Hiyo ni kweli. Na kama likitukia, basi mshukuruni Mungu, Roho wa Mungu yuko miongoni mwenu. Mnaona? Sasa, hapo ndipo mnapaswa kuwa makini na kuwa waangalifu. Kwa hiyo, msijaribu kujisukumiza. Singeweza kujifanya kuwa na macho ya hudhurungi wakati nina ya samawati, mnaona, sina budi kuridhika na macho ya samawati. Sasa, hapo ndipo ambapo pepo hutenda kazi katika ulimwengu wa watu wa kiroho.

⁷⁹ Sasa tuna jambo lenye kilindi sana linalokuja hapa, nami ninatumaini lisije likawa ni la kilindi sana. Sasa hapa katika Samweli wa Kwanza 28, ninataka kusoma Maandiko machache hapa wakati uu huu. Ninawatekeni msikilize kwa makini. Nami ninataka kuleta “pepo,” niwaonyeshe jinsi wanavyofanya kazi humo humo kanisani, na jinsi Shetani alivyo na uigizaji wa kila kitu halisi kilichopo. Sasa mnaweza kuona, kulingana na Biblia, ya kwamba pepo huja miongoni mwa Wakristo na wanaiga.

⁸⁰ Na mara nyingi tunawatangaza watu kuwa Wakristo wakati waliposema, “Ninamwamini Yesu Kristo.” Mbona, pepo wanaamini jambo lile lile, na kutetemeka. Hiyo siyo ishara umeokolewa. Moja ya siku hizi usiku nataka kuingilia uteuzi’ na halafu basi mtaona wokovu unamaanisha nini. Mnaona? Si jambo uliloweza kufanya juu yake, kwanza, ama mwishowe, wala lo lote unaloweza kufanya juu ya jambo hilo. Mungu humwoko mwanadamu, bila masharti. Ee walla, limezama ndani kina kirefu, sivyo? Sasa, afadhali litoke kwenye mfumo wenu, wakati tungali tuko kwenye jambo hilo. Vema.

⁸¹ Ibrahimu alikuwa chanzo cha imani yetu. Hiyo ni kweli? Loo, Ibrahimu alikuwa na ahadi. Na Mungu alimwita Ibrahimu kwa sababu alikuwa ni mtu mashuhuri, nadhani? La, bwana. Yeye alishuka akaja kutoka Babeli, katika—katika nchi ya Ukaldayo, katika mji wa Uru, ndipo Mungu akamwita na kufanya agano naye, bila masharti. “Nitakuokoa. Na si wewe tu, Ibrahimu, bali Uzao Wako,” bila masharti.

⁸² Mungu alifanya agano na mwanadamu, na mwanadamu huvunja agano lake kila mara. Mwanadamu hakuwahi kamwe kudumisha agano na Mungu. Torati haikushikwa kamwe. Hawakuweza kuishika torati. Kristo akaja na akavunja torati, Yeye Mwenyewe, maana neema tayari ilikuwa imetoa Mkombozi. Musa aliandaa njia ya kuokoka, na halafu ule wokovu, hasa, halafu hao watu, baada ya hapo, bado walitaka jambo fulani la kufanya. Mwanadamu daima anajaribu kufanya jambo fulani kujiokoa mwenyewe, ambapo huwezi kufanya jambo hilo. Ni asili yake. Mara alipojikuta yu uchi, katika bustani ya Edeni, alitengeneza aproni za majani ya mtini. Hiyo ni kweli? Lakini akakuta kwamba hazifai kitu. Hakuna kitu anachoweza kufanya mwanadamu kujiokoa mwenyewe. Mungu hukuokoa, bila masharti, katika miaka yote. Na halafu unapookolewa, umeokolewa.

⁸³ Mwangelie Ibrahimu. Huyu hapo huyo jamaa, akaenda kule, Na Mungu alimpa nchi ya Palestina na akamwambia asiondoke humo. Myahudi ye yote anayeondoka Palestina amerudi nyuma. Mungu alimwambia akae kule. Kama Mungu akikwambia ufanye jambo lo lote lile, nawe hulifanyi, umerudi nyuma. Hiyo ni kweli? Vema, ukame ukaja, kuijaribu imani ya Ibrahimu. Na badala ya Ibrahimu kukaa humo, la, hakuweza kukaa humo, alitoroka, na akamchukua Sara na kusafiri kama maili mia tatu (laiti ningalikuwa na wakati wa kuliendea jambo hilo) kwenye nchi ya ugeni.

⁸⁴ Na wakati alipofika kule, na basi akampata mfalme huyu mkuu kule, Abimeleki. Alikuwa kijana naye alikuwa anatafuta mchumba, kwa hiyo akampata mke wa Ibrahimu, Sara, na akampenda. Ndipo Ibrahimu akasema, “Sasa, wewe mwambie ya kwamba wewe u dada yangu nami ni kaka yako.”

⁸⁵ Kwa hiyo jambo hilo likampendeza Abimeleki, kwa hiyo akasema, “Vema, tutampeleka sasa hivi kwenye jumba la mfalme.” Nami nafikiri wanawake walimwandaa, naye alikuwa amwoe kesho yake.

⁸⁶ Naye Abimeleki alikuwa ni mtu mzuri, mtu mwenye haki. Na usiku huo, wakati alipokuwa amelala, Bwana akamtokea na kusema, “Wewe ni kama mtu aliyekufa.” Akasema, “Nanii wa mtu huyo. . . Mwanamke uliye naye huko upate kumwoa, ni mke wa mtu mwingine.” Sasa angalia.” Mke wa mtu mwingine.”

⁸⁷ Mbona, yeye akasema, “Bwana, wewe unajua unyofu wa moyo wangu,” mtu mwenye haki, mtakatifu. “Wewe unajua unyofu wa moyo wangu. Mtu huyo aliniambia ya kwamba huyo alikuwa ni ‘dada’ yake. Na je! mwanamke huyu hakuniambia, yeye mwenyewe, ya kwamba huyo alikuwa ni ‘ndugu yangu’?”

⁸⁸ Akasema, Mungu akasema, “Nilijua unyofu wa moyo wako, na hiyo ndiyo sababu nilikuzuia usinitendee dhambi. Lakini huyo ni nabii Wangu!” Haleluya!

⁸⁹ Yeye alikuwa kitu gani? Amerudi nyuma, na maskini mdanganyifu asiyeaminika. Hiyo ni kweli? Loo, la, hakuna uongo mdogo mweupe. Aidha ni uongo mweusi ama si uongo hata kidogo. Mtu huyo amaketi huko akisema uongo mweusi kabisa, akisema huyo alikuwa ni “dada” yake wakati alikuwa ni mkewe, akiepa ukweli, na amerudi nyuma.

⁹⁰ Na hapa palikuwa na mtu mwenye haki amesimma mbele za Mungu, na akasema, “Bwana, Wewe unaujua moyo wangu.”

⁹¹ “Pamoja na hayo sitayasikia maombi yako, Abimeleki, lakini mtwae mtu huyo. . . mrudishe mwanamke huyo na mtu huyo na akuombe. Yeye ni nabii Wangu; nitamsikia.” Naam, mtu aliyerudi nyuma, mwongo, lakini, “Huyo ni nabii Wangu.” Hiyo ni kweli? Hiyo ni Biblia.

⁹² Sasa, usiende mbali sana hapa kwenye upande wa Ukalvini, “Mara ukiwa katika neema, daima uko katika neema,” maana utaingia kwenye aibu. Unaona? Sasa, hebu kidogo, tutapata nafasi juma hili kulileta hilo na kuwaonyesheni jinsi lilivyo sawa. Lakini usifikirie ati kwa sababu tu umefanya kosa fulani ya kwamba umepotea milele. Wewe ni mwana wa Mungu, umezaliwa kwa Roho wa Mungu, ninyi ni wana na mabinti za Mungu, na matunda yatajishuhudia yenyewe. Hivyo ndivyo ilivyo.

⁹³ Sasa, tumefika, tumeketi katika ile nchi. Sasa, ninataka kusoma hapa, aya ya 6.

Lakini Sauli alipouliza kwa BWANA, BWANA hakumjibu, wala kwa ndoto, wala kwa Urimu, wala kwa nabii.

Ndipo Sauli akawaambia watumishi wake, Nitafutieni mwanamke mwenye pepo wa utambuzi, nipate kumwenda na kuuliza kwake.

Ningeweza kugusia jambo muhimu sana hapa, kwa ninii tu... "Nitafutieni mwanamke mwenye pepo wa utambuzi."

...Mtumishi wake akamwambia, Tazama, yuko mwanamke mwenye pepo wa utambuzi katika Endori.

Basi Sauli akajigeuza, akavaa juu ya vazi, vazi jingine, kisha akaenda, wawili...yeye na watu wawili pamoja naye, wakamfikilia yule mwanamke usiku; nao wakasema Tafadhali...-nibashirie kwa utambuzi, ukanipandishie yeye nitakayemtaja kwako.

Yule mwanamke akamwambia, Angalia, unajua alivyofanya Sauli, unajua jinsi alivyowakatilia mbali hao wenye pepo wa utambuzi na wachawi katika nchi; basi wanitegea tanzi uhai wangu, ili kuniua?

Naye Sauli alijibu, akamwapia kwa BWANA, akasema, Aishiryo BWANA, haitakupata adhabu yo yote kwa jambo hili...

Ndipo yule mwanamke aliposema, Je! ni nani nitakayekupandishia?...Naye akasema, Nipandishie Samweli.

Hata yule mwanamke alipomwona Samweli, alilia kwa sauti kuu; na yule mwanamke akamwambia Sauli, akisema, Mbona umenidanganya? kwa kuwa wewe ndiwe Sauli.

Mfalme akawambia, Usiogope: waona nini? Yule mwanamke akamwambia mimi...akamwambia Sauli, Naona miungu inatoka katika nchi.

Naye akamwuliza, Ni mfano wa nini? Akajibu, Ni mzee anazuka; naye amefunikwa vazi. Basi Samwe-... (Hilo ni lile vazi la nabii, bila shaka. Mnaona?). ... akatambua ndiye Samweli mwenyewe, akainama uso wake mpaka nchi, akasujudia.

Ndipo Samweli alimwambia Sauli, Mbona umenitaabisha mimi, hata ukanipandisha juu? Sauli akajibu, na akasema Mimi nimetaabika sana; kwa kwa maana hao Wafilisti wananifanyia vita, naye Mungu ameniacha; hanijibu tena, wala kwa nabii, wala kwa ndoto; kwa hiyo ni-...kuita wewe, ili wewe unijulishe nifanye nini.

Samweli akasema, Kwa nini kuniuliza mimi, akiwa BWANA amekuacha, naye amekuwa adui yako?

Yeye BWANA amekutenda kama alivyosema kwa kinywa changu; BWANA amekuraulia ufalme mkononi mwako, na kumpa jirani yako, yaani Daudi.

⁹⁴ Sasa, wengi wenu, mnajua jambo hili. Sasa tunataka kuingilia jambo hilo moja kwa moja, na Mungu atusaidie

sasa, kwa dakika chache, tuingie kwenye jambo hili. Sasa angalieni. Kulikuweco na mtu fulani, Sauli, ambaye wakati mmoja alidhaniwa kwamba ni nabii, kwa kuwa alitabiri pamoja na manabii. Je! hilo ni kweli, waalimu? Sasa, hapa mtu huyo alikuwa amerudi nyuma. Ni kweli? Lakini kumbuka mahali ambapo Samweli alisema angekuwa, pamoja naye, kesho yake. Ameondoka kabla ya wakati wake, unaona. Vema, kama hutamjali Mungu, Mungu atakuondoa duniani.

⁹⁵ Angalia katika barua ya Wakorintho pale, jinsi Paulo alivyowaweka hao watu katika utaratibu. Alisema, “Kwanza, Ninamshukuru Mungu kwa ajili yenu, ya kwamba hakuna mambo kama hayo kati yenu, na kadhalika, na jinsi ambavyo—ambavyo hampungukiwi na karama yo yote ya roho.” Akiwaambia kile walichokuwa, mahali pao, katika Kristo. Halafu kaanza kuwatwanga nyundo, kuwaambia juu ya wanawake wao wahubiri, na jinsi walivyokuwa wanafanya, na jinsi walivyokuwa wakila kwenye meza ya Bwana.

Na hata mtu mmoja akiishi na mama yake wa kambo, naye akamwambia mtu huyu katika Kristo, “Mtoleeni Ibilisi, ili mwili wake uharibiwe, ili roho yake iokolewe.” Mnaona, hivyo ndivyo ilivyo, mtoleeni. Biblia ilisema, “Kwa ajili hii wengi hawawezi na ni wadhaifu, na wengi wamelala,” wameondoka kabla ya wakati wao kwa sababu ya dhambi. Mungu anakuondoa; ishara nzuri ya kwamba wewe ulikuwa ni Mkristo, kama uliondolewa.

⁹⁶ Kwa hiyo, sasa angalia hapa, Sauli alihesabiwa mmoja wa manabii, ama miongoni mwa manabii, kwa sababu alitabiri. Na sasa alikuwa amerudi nyuma, kwa sababu hakumtii Mungu, na ufalme wake ukaondolewa mikononi mwake na kuwekwa mikononi mwa Daudi, ambaye Mungu alikuwa amemtia mafuta kwa mkono wa Samweli, kwa pembe ya mafuta.

⁹⁷ Angalia, basi, kulikuwa na njia tatu walizokuwa nazo za kupata mambo kutoka kwa Mungu; ya kwanza ilikuwa—ilikuwa ni nabii, ya pili ilikuwa ni ndoto, na ya tatu ilikuwa ni Urimu ya Thumimu. Wala hakuna iliyojibu. Sasa, mnajua nabii ni kitu gani, mnajua ndoto ya kiroho ni nini, na mnajua Urimu ya Thumimu ilikuwa ni nini. Mnajua, hivi majuzi nilimuuliza m—mtu fulani Urimu ni nini, na mtu huyu hakuweza kuniambia ilikuwa ni nini, ile Urimu ya Thumimu. Maana, ilikuwa ni Mungu akijibu kwa njia hizi. Mnaona?

⁹⁸ Naye Ibilisi anafanya uigizaji wa kila moja ya hizo; mchawi, nabii wa uongo, mnajimu. Mnaona?

Sasa, Urimu ya Thumimu ilining’inia kifufani mwa Haruni, *hapa*, na ile Urimu ya Thumimu ikafunika mawe hayo. Nao wakaitundika hekaluni. Na wakati hawakuwa na hakika, wangeenda mbele za Mungu, kupata jibu, na mwanga ungemulika kwenye Urimu hiyo ya Thumimu, ambapo, kama ilikuwa ni mapenzi ya Mungu, ama siyo. Sasa, wakati Urimu ya

Thumimu haikujibu. . . Sasa, hilo lilikuwa ni jibu la moja kwa moja la kutoka kwa Mungu.

Sasa, ile Urimu ya Thumimu ya leo; mpiga ramli alichukua jiwe la marmar la mviringo, apate kuigiza Hiyo; kitu cha uongo. Mungu yuko katika utatu; nguvu za Mungu ziko katika utatu. Na ibilisi yuko katika utatu, na nguvu zake ziko katika utatu. Nami ninaweza kuthibitisha jambo hilo kwa Biblia. Na hiyo Urimu ya Thumimu; ilikuwa tu ni ile marmar nyeupe ya mviringo ambayo Ibilisi hutumia siku hizi. Na huyo nabii wa uongo zamani hizi za leo, yule tuliye naye sasa, alikuwa. . . Ama, mchawi, ama mpiga ramli huko nje, alichukua mahali pa nabii, upande wa Ibilisi. Mnaona ninalomaanisha?

⁹⁹ Sasa, basi, ile Urimu ya Thumimu leo ni Biblia hii. Kama mtu ametoa unabii ama ndoto, nayo hailingani ama haitoi mwangwi wa Biblia ya Mungu, ni uongo. Usiuamini.

¹⁰⁰ Mtu fulani alinijia si muda mrefu uliopita, kutoka India, ambako ninajitayarisha kwenda, mhubiri mzuri mdogo. Akasema, “Ndugu Branham, nimekuja hapa.” Kasema, “Mwanamke fulani alikuwa na Roho Mtakatifu, na,” kasema, “alikuwa tu ni mwanamke mpole sana, mzuri sana.” Akasema, “Naye alikuwa ameolewa mara nne, naye alikuwa anaishi na mume wake wa nne. Nami nikasema, ‘Vema, hiyo ingewezekanaje, Bwana?’” Kisha akasema, “Nilimwendea nikasema, ‘Loo, Mungu atukuzwe’ Kasema, ‘Haleluya! Bwana asifiwe!’” Mmoja tu wa aina hiyo, unajua. Kasema, ‘Haleluya, Bwana apewe sifa!’” Kasema, “Bwana akaniambia, ‘Tazama, nitakupa ndoto.’” Naye akasema, “Niliota ya kwamba mke wangu, nilimwona akiishi katika uzinzi. Basi akarudi kwangu na kusema, ‘Jamani, utanisamehe, Victor? Utanisamehe? Mimi sikuninii. . .’ ‘Mbona,’ nikasema, ‘hakika, nitakusamehe na kukurudisha.’” Yule mtu akasema, “Sasa, hivyo ndivyo nilivyofanya.” Kasema, “Unaona, ninasamehe.”

¹⁰¹ Nikasema, “Victor, ndoto yako ilikuwa nzuri sana, lakini ulipewa hiyo na Ibilisi.”

Akasema, “Kwa nini?”

¹⁰² Nikasema, “Hailingani na Neno la Mungu. Yeye anaishi katika uzinzi. Kabisa. Yeye hawezi kuishi na wanaume wanne. Kweli. Akimwacha huyu na kumrudia yule wa kwanza, yeye ni mbaya zaidi kuliko alivyokuwa hapo mwanzo. Hana budi kuishi peke yake, maishani mwake mwote.” Nikasema, “Unajua hiyo hailingani na Neno la Mungu. Kwa hiyo ninii ya huyu mama. . . Ndoto yako ilikuwa ni ya uongo.” Nikasema, “Haitalingana na Hili.”

¹⁰³ Na wakati nabii alipotoa unabii, wao walinena, na walitaka kuona kama unabii huo ulikuwa ni wa kweli, waliuweka mbele ya Urimu ya Thumimu. Na kama Sauti ya Mungu ilitupa ile mianga ya Urimu ya Thumimu, basi ilikuwa ni mkataa, ni ile

Kweli. Na kama mtu akitoa tafsiri, akitoa ndoto, akitoa kitu fulani cha Biblia, na, ama kitu cho chote kile, wala hakilingani na Biblia ya Mungu, ni uongo. Hiyo hapo Urimu ya Thumimu ya leo. Neno la Mungu hunena, na hiyo ni Sauti ya moja kwa moja ya Mungu, kama vile Urimu ya Thumimu ilivyokuwa kabla Biblia haijaandikwa. Amina! Haleluya! Ninajisikia wa kidini kwa namna fulani sasa hivi. Msinichukulie ni mshupavu wa dini, kama mkifanya hivyo. Ninajua. Ninajua mahali nilipo. Sikuchemka. Hiyo ni sawa.

¹⁰⁴ Kweli iko hapa, Neno la Mungu! Sijali ulipata ndoto ya namna gani, ama ulitoa unabii wa namna gani, kama si Neno la Mungu. Ni kosa kama haulingani na Neno hilo. Hiyo ndiyo shida ya siku hizi. Mmoja ana ndoto, mmoja ana ono, mmoja ana lugha, mmoja ana ufunuo; imelifanya jambo hilo lote kuchafuliwa na kila kitu, mna madhehebu na mkavunja kila kitu. Mnapaswa kulirudisha kwenye msingi wa mwisho, na huo ni Neno la Mungu. Hiyo ni kweli.

¹⁰⁵ Makanisa yamejengwa juu ya mmoja, unasema, “Tazama, Yesu yuaja juu ya farasi mweupe. Najua. Nilimwona katika ono.” Wanaunda kanisa la namna hiyo. “Loo, haleluya! Yeye yuaja kwa wingu.” Wanaunda la namna hiyo. Wanayavunja, na kutengana, na kuitana “Kiota cha mwewe,” na “nyumba ya chawa,” na cho chote kile. Mbona, ndugu, inaonyesha, kwanza, moyo wako hauko sawa na Mungu unapofanya jambo hilo. Hiyo ni kweli. Sisi ni ndugu. Hatuna budi kushikamana. Mmoja anamhitaji mwingine.

¹⁰⁶ Sasa angalia. Sauli alikuwa amerudi nyuma, naye anapanda anaenda. Yeye, Mungu, alikuwa amemwacha. Ndipo akapanda akaenda akataka shauri kwa manabii. Hao manabii wakatoka wakaenda na kujaribu kutoa unabii, na ndipo Mungu akakata mawasiliano, hangetoa ono. Nabii akatoka akaja, kasema, “Siwezi. La. Yeye hajaniambia jambo lo lote juu yako.”

¹⁰⁷ Vema, ndipo akasema, “Bwana, nipe ndoto.” Usiku baada ya usiku, hakuna ndoto iliyokuja.

¹⁰⁸ Ndipo anaenda kwenye Urimu ya Thumimu, na akasema, “Ee Mungu! nimewajaribu manabii, nimejaribu ndoto, sasa nisaide. Utanisaidia?” Akakata mawasiliano, hakuna Mwangi uliomulika hata kidogo.

¹⁰⁹ Ndipo akaenda mchawi, kitu cha hali ya chini, kitu cha aibu. Basi akamwendea, naye akatambaa akaingia na kujibadilisha. Naye huyu machawi anaondoka na anaenda kuita roho ya Samweli.

¹¹⁰ Sasa, najua mnayowazia. Wengi walisema, “Huyo hakuwa Samweli.” Lakini Biblia ilisema ilikuwa ni Samweli, na ilikuwa ni Samweli. Ni ajabu jinsi unavyoshika jambo hilo, sivyo? Lakini huyo alikuwa ni Samweli. Biblia ilisema ilikuwa ndiye.

¹¹¹ Na huyo mchawi angeweza kumwita, naye akamwita Samweli. Na Samweli alikuwa mahali pengine, lakini alikuwa ana fahamu na yale yaliyokuwa yakiendelea, na alikuwa bado amesimama amevaaa vazi lake la nabii. Kwa hiyo, ndugu, wakati unapokufa, wewe hukufa, unaishi mahali fulani, mahali pengine.

¹¹² Hebu nisimame kwa dakika moja tu, kuelezea hii elimu ya pepo kidogo tu. Yule mwanamke alikuwa ni pepo, lakini alikuwa na mawasiliano ya karibu na ulimwengu wa roho. Sasa, leo, kwa kweli kuna waamini mizimu wengi wanaojua mengi kweli kuhusu ulimwengu wa roho kuliko watu wanaokiri wenyewe kuwa ni Wakristo, na hata hivyo yeye ni pepo. Katika nyakati za Biblia lilikuwa ni jambo lile lile.

¹¹³ Wakati Yesu alipokuwa hapa duniani, kulikuwako na hao maprofesa na wasomi na waalimu, baadhi ya walio bora sana waliokuwepo, tokea kwenye seminari bora zaidi kuliko ambazo tungeweza kuanzisha leo. Na ni watu watakatifu, watu wenye sifa, iliwabidi kuwa hivyo. Kama Mlawi alipatikana, ilibidi aonekane asiye na lawama, mwenye haki kwa kila hali. Na hata hivyo mtu huyo hakujua zaidi juu ya Mungu kuliko sungura alivyojua kuhusu viatu vya theluji. Wakati Yesu alipokuja, yeye alishindwa kumtambua, naye alimwita Yesu ni “pepo.” Alisema, “Yeye ni Beelzebuli, mkuu wa Pepo.” Hiyo ni kweli?

¹¹⁴ Na hapa kukaja pepo wa hali ya chini sana, aliyekuwa amemfunga mtu kule makaburini, na kila kitu, nao wakamwita. Pepo mwenyewe akasema, “Tunajua wewe ni nani. Wewe ni Mwana wa Mungu, Yule Mtakatifu.” Hiyo ni kweli? Wachawi na walozi, pepo, walimtambua kama Mwana wa Mungu; wakati watu walio na elimu, wahubiri wa seminari za theolojia walimtambua Yeye kama Beelzebuli. Ni nani walijua kweli, pepo ama mhubiri? Pepo. Na, ndugu, mambo hayajabadilika sana leo. Watu hawatambui nguvu za Mungu.

¹¹⁵ Haidhuru umepata mafundisho kiasi gani, unaweza kuyashindilia ndani yako. Mungu hayuko kwenye maneno makubwa makubwa. Mungu yuko katika moyo mwaminifu. Wewe unaweza kusimama hapa, uzungumze maneno makubwa, kama vile sijui kitu gani, hayo hayakuleti karibu na Mungu. Unaweza kusimama na kujifunza jinsi ya kurudia mahubiri yako na kusema mambo haya, hilo halikuleti karibu na Mungu. Unaweza kujifunza kamusi mpaka unalala na moja, na bado jambo hilo halingalikuleta karibu na Mungu. Moyo mnyenyekevu, uliosalimishwa, katika unyofu, ndio unaokuleta kwa Mungu. Na hiyo ni kweli. Amina! Moyo mnyenyekevu, Mungu anaupenda. Sasa, haidhuru kama hujui ABC zako, hilo halileti tofauti yo yote. Moyo mnyenyekevu tu! Mungu hudumu katika moyo mnyenyekevu; si katika elimu, si katika mashule, si katika theolojia, maseminari, si katika sehemu hizi nyingine zote mbalimbali; si katika maneno makubwa makubwa, wala

si katika sehemu za hali ya juu. Mungu anakaa ndani ya moyo wa mwanadamu. Na jinsi unavyoweza kujidhili chini, jinsi unavyozidi kuwa mnyenyekevu, unaweza kuwa mkuu zaidi machoni pa Mungu.

¹¹⁶ Hebu niwape jambo fulani. Ninaona mashamba yenu yamejaa ngano huku nje. Kichwa cha ngano iliyokomaa vizuri daima huinama. Maskini mmea uliokomaa hutokeza juu huko, na kutikisika-tikisika kama kwamba unajua kila kitu, hauna cho chote kichwani. Hivyo ndivyo ilivyo kwa wengi wa jamaa hawa wanavyofikiri wana mengi sana kichwani mwao, wala hawana kitu moyoni mwao. Ama, kichwa kitakatifu kitasujudia Nguvu, kitamtambua Yesu Kristo kama Mwana wa Mungu, na kuamini kazi Zake.

¹¹⁷ “Naye ni yeye yule, jana.” Loo, wao wanamtambua, hakika, katika mwelekeo wa kihistoria. Lakini si jambo la kihistoria. Watu wanasimama na kusema, “Loo, ninaamini Pentekoste, walipokuwa na kushukiwa kukuu na mambo kama hayo,” na kuchora moto. Mtu anayeganda kwa baridi hawezi kupata joto kwa moto wa kuchorwa. Moto wa kuchorwa hautii mtu joto. Hivyo ndivyo walivyokuwa. Ni kitu gani leo, kama Yeye ni yeye yule jana, leo na hata milele? Huo ni moto wa kuchorwa. Jamaa fulani akifa kwa baridi, aseme, “Angalia ule moto mkubwa waliokuwa nao.” Mbona, huo haukutii joto.

¹¹⁸ Walichofanya kule Pentekoste, walichokuwa nacho katika Agano la hapo awali, tunacho sasa! Na mara Mungu anapoweza kulinyosha jambo hilo, na Kanisa limewekwa pamoja, Kunyakuliwa kutakuja. Lakini hata hatuwezi kupata imani kwa ajili ya kuponya Kiungu, sembuse Kunyakuliwa, kwa sababu sote tumechanganyikiwa, mmoja upande *huu* na mwingine upande *ule*. “Na Dakitari *Fulani* alisema ilikuwa ni *hivi*. Vema, mhubiri wangu alisema Yeye alikuwa Hivi.”

¹¹⁹ Muda kidogo uliopita, mwanamke fulani alisema, “Yeye ni mwigaji tu.” Kasema, “Kasisi wangu aliniambia hivyo.” Ningetamani kasisi wake angeshuka aje hapa wakati mmoja, tungeona ni nani aliyekuwa mwigaji. Naam. Vema. Tutaona ni nani aliye mwigaji. Njoni mjaribu.

¹²⁰ Hapa si muda mrefu uliopita, Harlingen, Texas, tulikuwa na ibada huko. Nao walikuwa na maandishi makubwa, kote kote kwenye magari usiku huo nilipoenda kule, yakisema ya kwamba FBI walikuwa wanataka kunifichua kama mwongo. Kwa hiyo maskini msichana mdogo alikuwa ameponywa kule Texas mahali fulani kule. Alikuwa anatoka, na, na—nadhani, karibu maili elfu moja, huko mbali karibu na Panhandle. Na hapa ilikuwa huku mbali Harlingen, chini huko mpakani. Ndugu Baxter akaja, akasema, “Ndugu Branham,” kasema, “hujapata kuona mchafuko huko chini, yapata watu elfu nne ama elfu

tano.” Kisha akasema, “Halafu, kila mahali, FBI itakushika jukwaani usiku wa leo, na kukufichua.”

Nikasema, “Vema, bila shaka ninafurahia jambo hilo.”

¹²¹ Akasema, “Unajua yule msichana mdogo aliyeponywa hivi majuzi usiku?”

¹²² Nilikuwa nikitoka nyumbani nikitokea...nikienda chumbani kwangu. Nikasikia kitu fulani kinalia, nami nikaangalia huku na huko. Nilidhani labda mtu fulani alikuwa amevamiwa. Ilikuwa ni msichana fulani. Nami nikaangalia nyuma. Nikasema...Ndipo nikarudi, nikasema, “Kuna nini, Mama?” Na ilikuwa ni wasichana wawili waliokuwa wamesimama pale, wenye umri wa kama miaka kumi na saba, kumi na minane, kila mmoja, wamekumbatiana, wanalia.

¹²³ Kasema, “Ndugu Branham!” Nilijua basi walinijua. Kasema, “Sisi, nilimleta umbali wote huu hapa.” Kasema, “ilibidi apelekwe kwenye hospitali ya wenda wazimu.” Na maskini msichana huyo mdogo alikuwa kwenye mkutano wangu huko Lubbock, Texas. Ndipo akasema, “Nilijua kama ningeweza kumleta huku nawe umwombee, ninaamini Mungu angemponya.”

¹²⁴ Vema, nikawaza, “Ni imani ya namna gani!” Ndipo nikasema, “Vema, sasa, dada, unaweza kumleta...” Na wakati uo huo basi nikasema, “Mlikuja huku kwa gari la manjano, sivyo?”

Kasema, “Ndio!”

Kisha nikasema, “Mama yako ni kiwete.”

Akasema, “Hiyo ni kweli.”

Nikasema, “Wewe ni mfuasi wa kanisa la Kimethodisti.”

Akasema, “Hiyo ni kweli kabisa.”

¹²⁵ Ndipo nikasema, “Mlipokuwa mkija barabarani, nusura mpinduke. Wewe na msichana huyu mlikuwa mnacheke wakati mlipokuja karibu na mahali palipokuwa nusu saruji na nusu lami, na mlikuwa mkikata kona.

Akasema, “Ndugu Branham, hiyo ni kweli!”

Nikasema, “Na, BWANA ASEMA HIVI, msichana huyo ameponywa.”

¹²⁶ Kesho yake alikuwa akiuwasha mji, akimwambia kila mmoja, akienda kila mahali kutangaza jambo hilo. Hapana shaka, wao hawakumjua kule, kama alipata kuwa katika hali hiyo ama la. Na halafu siku hiyo mimi...Ndugu Baxter akasema, “Ndugu Branham,” kasema, “hao wasichana wako kule wakifungasha nguo zao kwenye sanduku lao.” Na hili ni jambo moja ambalo hakujua ya kwamba nilijua. Fedha zilikuwa zimetuishia kabisa. Sikumruhusu azungumze juu ya jambo hilo. Lakini mmoja wa hao wasichana aliweka dola mia tisa kwenye—

kwenye hiyo sadaka usiku uliotangulia, na kuinua hali ile ya fedha. Sasa, yeye ndugu hakujua, yeye hajui jambo hilo mpaka leo, lakini mimi nilijua. Mnaona? Ya kwamba mimi... Mungu aliniambia mambo yote yatakuwa ni mazuri.

¹²⁷ Basi Ndugu Baxter akasema, “Ndugu Branham,” kasema, “afadhali uniruhusu nitoe ushawishi mdogo.” Kasema, “Wamekuwa na baadhi ya hawa waponyaji wa Kiungu hapa ambao waliwashawishi tu hawa watu.”

¹²⁸ Nikasema, “Hata kidogo. La, bwana. Hutafanya jambo hilo. Ndugu Baxter, wakati wote utakapowashawishi upate pesa namna hiyo, huo ndio wakati mimi na wewe tutapeana mikono kama ndugu, nitabaki peke yangu. Mnaona?” Nikasema, “Usifanye hivyo.” Nikasema, “Mungu anamiliki ng’ombe juu ya milima elfu, na kila kitu ni mali Yake. Mimi ni mali Yake. Yeye atanishughulikia mimi.”

Yeye akasema, “Vema.”

¹²⁹ Na usiku uo huo yeye akasema, “Ndugu Branham, angalia hapa. Mtu fulani... Angalia! Hii hapa bahasha, haina jina juu yake, ina noti za dola mia tisa ndani. Ni zile tu hasa tunazohitaji kulipia madeni.”

Nikasema, “Ndugu Baxter.”

Akasema, “Nisamehe.”

¹³⁰ Kwa hiyo basi nilijua ilikuwa ni msichana huyo. Kwa hiyo basi—basi kesho yake, Ndugu Baxter akasema, “Ndugu Branham, wao wako kule wakifungasha nguo zao, wanalia.”

Nikasema, “Kuna nini?”

Kasema, “Afadhali ushuke uende ukawaone.”

¹³¹ Nilishuka nikaenda kwenye chumba walimokuwa. Nikasema, “Wako kwenye chumba gani?” Nikaenda nikapiga hodi mlangoni. Nikawasikia wakilia. Nikagonga mlango, na msichana huyo akaja mlangoni, akasema, “Jamani, Ndugu Branham, ninasikitika sana.” Akasema, “Nimekusababishia matatizo yote haya.”

Nikasema, “Ati matatizo? Kuna nini, dada?”

Akasema, “Loo, nimewafanya FBI wakufuatilie.”

Ndipo nikasema, “Loo, hiyo ni kweli?”

¹³² Kasema, “Ndio.” Kasema, “Nafikiri nilishuhudia sana kupita kiasi mjini leo, na kila kitu.”

Nikasema, “La.”

¹³³ Naye akasema, “Ndugu Branham, FBI wako upande ule, wako kule, wanakuja kukufichua usiku wa leo.”

¹³⁴ Nikasema, “Vema, kama mimi—kama mimi ninafanya kosa lo lote, ninapaswa kufichuliwa. Unaona?” Nikasema, “Hakika. Kama kuhubiri Injili kunapaswa kufichuliwa, vema,

na tukufichue. Mnaona?” Nikasema, “Na—na—naishi kwa Biblia hii, na kile ambacho Biblia hii haisemi. . . Hii ndiyo kinga yangu, papa hapa. Mnaona?” Nami nikasema, naye. . .

Akasema, “Vema,” kasema, “Ninasikitika tu ya kwamba nilifanya nililofanya.”

Nikasema, “Hukufanya kitu, dada. ”

Akasema, “Vema, huogopi kwenda huko?”

Nami nikasema, “La.”

Akasema, “Vema, FBI wako huko.”

¹³⁵ Nikasema, “Vema, wamehudhuria mkutano wangu siku za nyuma na wakaokolewa.” Nikasema, “Bw. Al Ferrar. . .”

¹³⁶ Kapiteni Al Ferrar, wengi wenu mnajua habari za kuongoka kwake kule Tacoma, Washington, aliokolewa, kule kule chini kwenye chumba cha kulenga shabaha. Alikuwa mkutanoni, akasema, “Nimemfuatilia mtu huyu kwa miaka miwili. Nami nilisikia habari za fedha, nami nimezichunguza, na nilipitia kila mahali.” Ndipo akasema, “Ni Kweli, hamumsikilizi mshupavu wa dini usiku huu, mnasikiliza Kweli.” Kasema, “Mtu mmoja kwenye jeshi la polisi, ambaye mtoto wake nilimpeleka akachunguzwe na daktari kisha nikampeleka kwenye mstari wa maombi,” na akasema, “mtoto huyo aliambiwa shida yake ilikuwa ni nini hasa, na nini kilichompata. Naye akasema, ‘Katika muda wa siku nane, atakuwa amerudi shuleni, ugonjwa wa polio.’” Ndipo akasema, “Katika siku ya nane mtoto huyo akarudi shuleni.” Kasema, “Mimi nimemfuatilia kwa muda wa miaka miwili,” mbele ya watu elfu kumi. Hayo yote pale. . . Hiyo hapo picha yake, ule mkutano wa Seattle, katika—katika kitabu chenu. Akasema, “Ninataka ninyi nyote mjue ya kwamba hamumsikilizi mwanadini wa bandia. Mnasikiliza Kweli.” Kapiteni Al Ferrar. Na kesho yake nikamwongoza kwa Mungu, naye alipokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, katika chumba cha kulengea shabaha, kule chini kwenye mahali pale pakubwa kule.

Nikasema, “Labda jamaa huyu atafanya jambo lile lile.”

Kwa hiyo yule msichana kasema, “Unaogopa kwenda huko?”

¹³⁷ Nikasema, “Eti kuogopa? Mbona, bila shaka siogopi. Bila shaka siogopi. Kwa nini niogope wakati Mungu alinituma kufanya jambo hilo? Yeye Ndiye anayepigana hivyo vita, si mimi.” Kwa hiyo nikasema, “Sasa, ninataka ninyi nyote mkae kando.” Na kwa hiyo. . .

¹³⁸ Tukaenda kwenye mkutano usiku huo, mahali pale palikuwa pamejaa watu. Ndipo mlinzi wa mahali pale akatoka, akasema, “Kasisi Branham, nimewaajiri watoto kumi wa Kimeksiko.” Kasema, “Angalia hapa, ‘Kasisi Branham kufichuliwa usiku wa leo na FBI, mshupavu wa dini,’” ama kitu kama hicho.

Kisha akasema, “Yako kwenye kila moja ya hayo magari. Wakayatoa...” Kasema, “Niliwaajiri watoto wadogo kumi wa Kimeksiko, kwenda wakayabandue yote na kuyaweka hapa.” Kasema, “Loo, ninajisikia kama laiti ningalimshika jamaa huyo!”

¹³⁹ Nikasema, “Usitie shaka, bwana. Mungu atamshika, unaona.” Nikasema, “Mwache tu.”

¹⁴⁰ Kwa hiyo akaja. Na usiku huo wakati tulipoingia, sitasahau kamwe, nikaingia kwenye kile chumba. Mimi... Ndugu Baxter akaimba *Amini Tu*. Akasema, “Sasa, Ndugu Branham anasema usiku wa leo tutoke kwenye jengo.” Kasema, “Mimi nitaenda kule nyuma kabisa nikaketi chini.” Akasema, “Wanajitayarisha kumfichua usiku huu hapa jukwaani.” Akasema, “Mimi nimemwona katika vita vingi vikali, na kuona Mungu akimpigania.” Kasema, “Mi—mimi ninarudi tu kwenda kuketi chini.”

¹⁴¹ Nikaenda kule. Nikasema, “Nilikuwa ndio tu nisome makala ndogo hapa ambapo ningefichuliwa usiku wa leo hapa jukwaani.” Nikasema, “Nataka hao maajenti wa FBI sasa waje mbele wakanifichue hapa jukwaani.” Nikasema, “Ninasimama hapa kuitetea Injili; ninataka mje mnifichue.” Nikangojea. Nikasema, “Labda bado hawajafika.” Nilijua mahali nilipokuwa. Yeye alikuwa tayari amenionyesha chumbani mwangu kule, mambo yatakayotukia, kabla sijaondoka, mnaona. Nami nikasema, nikasema, “Labda nitangojea kidogo tu. Twaweza kuimba wimbo?” Na mtu akapanda akaja akaimba wimbo wa mtu mmoja.

¹⁴² Nikasema, “Bw. ajenti wa FBI, uko ndani ama uko nje? Mimi ninangojea kufichuliwa. Unaweza kujitokeza?” Hakuna mtu aliyekuja. Nikawa ninashangaa ilikuwa ni wapi. Bwana alikwisha kuniambia kwamba ilikuwa ni nini. Ilikuwa ni wahubiri wawili waliorudi nyuma, nami ni—nilikuwa nikiangalia. Niliona kivuli cheusi kinaning’inia kwenye kona. Niliona ilikuwa ni wapi. Nikaangalia hapo, nacho kikasogea kikapanda moja kwa moja kikaingia kwenye roshani namna hii. Mtu mmoja mwenye suti ya buluu, mmoja amevaa ya kijivu.

¹⁴³ Nikasema, “Enyi rafiki zangu, hakuna cha FBI. Hivi FBI wana uhusiano gani na kuhubiriwa kwa Biblia?” Nikasema, “Haina hata kidogo. Haikuwa ni FBI wawili wa kunifichua mimi. Lakini, huko kufichuliwa ndio huku, wale pale wameketi pale juu wazi wazi, hao wahubiri wawili wazi wazi pale.” Nao wakashuka. Nikasema, “Msitoroke namna hiyo.” Na majitu mawili ya Wateksasi walikuwa wanapanda waende kule na kuwashika kwa nguvu. Nikasema, “Hapana, ndugu, hili si jambo la mwili na damu, ketini kimya. Mungu atashughulikia jambo hilo.”

¹⁴⁴ Nikasema, “Sasa, ndugu, angalieni, wakati mngalipo huko juu, angalieni huku.” Nikasema, “Kama... Mlisema ya kwamba mimi nilikuwa Simoni mchawi, chini ya uchawi, nilikuwa nikiwaloga watu.” Nikasema, “Kama mimi ni Simoni mchawi, basi ninyi ni watu wa Mungu. Sasa shukeni mje hapa jukwaani. Na kama mimi nikiwa ni Simoni mchawi, Mungu na anieue. Na kama mimi ni nabii wa Mungu, ninyi shukeni mje na Mungu awaue. Sasa tutaona ni nani aliye wa kweli na ni nani wa uongo. Sasa shukeni mje. Tutaimba wimbo.” Haoo! wakakimbia nje ya jengo, wala hatujawaona tangu wakati huo. Mnaona? Nikasema, “Njoni. Kama mimi ni Simoni mchawi, hebu Mungu anipige nife. Na kama mimi ni nabii wa Mungu, basi Mungu atawaua mtakapokuja hapa jukwaani. Ikiwa mimi ni wa kweli mbele za Mungu, Mungu atawaulia hapa jukwaani.” Hawangethubutu. Hiyo ni kweli. Hawangethubutu. Walikuwa wamesikia kutoka mahali pengine. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo msifikiri kamwe ila kwamba Mungu ni Mungu. Yeye hujibu.

¹⁴⁵ Sasa, huyu mchawi wa Endori, aliita roho wa Samweli. Naye Sauli akanena na Samweli. Sasa, huenda mkashangaa jinsi jambo hilo liliweza kutendeka. Haliwezekani leo. La, bwana. Kwa sababu, damu ya mafahari na mbuzi ilikuwa inangojea tu wakati wa kutimizwa. Wakati mtu alipokufa katika siku hizo... Wahubiri, niungeni mkono kama mnafikiri ni kweli. Wakati mtu alipokufa, yeye alikufa chini ya upatanisho wa mnyama, na nafsi yake ilikwenda ikaingia Paradiso. Na hapo alikaa mpaka wakati huo, hata—hata Siku ya Ukombozi. Na nafsi yake ilikuwa huko.

¹⁴⁶ Hebu niwachoree picha ndogo hapa. Ni wangapi waliosoma makala yangu, ama makala waliyoandika habari zangu katika *Reader's Digest* hapa, kwenye makala ya labda Oktoba, toleo la Novemba? Vema. Je! mliona jinsi jambo hilo lilivyokuwa? Je! mliona, yapata majuma mawili matatu kabla ya hapo, huyu kijumbe ambaye amejaribiwa tangu muda mrefu uliopita, yeye, Bibi Pepper. Je! kuna mtu ye yote aliyepata kusoma hayo, makala ya Bi Pepper katika *Reader's Digest*? Je! si ni ajabu jinsi hizo roho mbili...

¹⁴⁷ Je! nina muda gani? Ni mdogo tu. Nimepitisha dakika ishirini; nitaharakisha tu. Ninajua mnaninii... Angalieni, samahani muda kidogo.

¹⁴⁸ Mnajua, kuna—kuna wa uongo. Kuna cha kweli na cha uongo kwa kila kitu. Kama nikikupa dola, nami niseme, “Je! hii ni dola nzuri?” Nawe ungeiangalia, na ingebidi ionekana zaidi sana kama dola halisi la sivyo hungeiamini. Hiyo ni kweli? Kwa hiyo haina budi kuwa ni bandia nzuri kweli.

¹⁴⁹ Na kama Yesu alisema roho hizo mbili katika siku za mwisho zingefanana sana hata zingewadanganya walio Wateule kama yamkini, watu wa kidini. Sasa kumbuka. Sasa, hakuna kitu huko nje kwa ajili ya hayo ninii ba-... kide-... ninii baridi, ya

kidesturi. Kwa nje wao wana mfano tu wa utauwa, mnaona. Lakini roho hizi mbili, roho halisi, zingefanana sana hata zingewapoteza walio Wateule, jinsi zilivyokuwa zikitenda kazi sambamba katika siku za mwisho. Je! Yesu hakusema jambo hilo? Alisema.

¹⁵⁰ Sasa angalia, enyi rafiki zangu, nitawachorea picha ndogo. Nawatakeni mwangalie hapa kidogo tu. Na mnisikilize kwa makini, maana naenda kuwapa mfano, na ndipo mtaelewa.

¹⁵¹ Sasa, katika *Reader's Digest*, imeandikwa kule, nilikuwa nimesimama pale, tulikuwa na watu elfu mbili mia saba wakingojea kuombewa, wamesimama kule nje. Mlisoma makala hayo. Ndipo mtu fulani akashuka akaja kutoka Kanada, naye alikuwa na mvulana mdogo aliyekuwa ametoka kwa Mayo na John Hopkins, ugonjwa mbaya mno wa ubongo ulioikunyata mikono yake namna *hii*, na kuikunyata miguu yake chini yake. Nao wakasema, "Hakuna hata upasuaji ama cho chote kile kinachoweza kufanyika."

¹⁵² Kwa hiyo akamrudisha Kanada. Akasema, "Sijashindwa bado." Hebu tafuta nakala ya Novemba ya *Reader's Digest*, na yanaitwa ule—ule Muujiza wa *Donny Morton*. Na—na halafu ikasema ya kwamba ile, ndani mle, ya kwamba mtu hu—huyo alisema, "Mimi sijashindwa bado, kwa maana ninamjua mponyaji wa imani anayelitwa William Branham, aliyewafanya marafiki wangu wawili waliokuwa viziwi na bubu kunena na kusikia."

¹⁵³ Nao wakapiga simu na kujaribu kupata mahali nilipokuwa, Ma—Marekani bado. Nami nilikuwa huko Costa Mesa, California. Na ni makala, utakapoyasoma, uwe tayari kulia. Yatakuhuzinisha sana tu. Jinsi alivyopitia kwenye mikondo ya theluji, na kila ghasia, akiwa na mtoto mdogo yule! Akasema, "Uwe mwangalifu, Donny." Kasema, "Sasa, hatujashindwa." Na maskini mvulana huyo mdogo hakuweza hata kutabasamu, isipokuwa kwa shida, alikuwa anateseka sana. Kasema, "Hatujashindwa, tutamwomba Mungu. Tutamwendea nabii wa Mungu na kumwuliza."

¹⁵⁴ Kwa hiyo wakapitia kwenye theluji. Na hatimaye wakafika kule, naye mama mzazi wa mtoto alikuwa akifuatana nao, nao hawakuwa na fedha za kutosha kwenda kwa ndege, kwa hiyo wakamrudisha mama nyumbani. Basi mvulana huyo na babaye ilibidi wasafiri kwa basi, na jinsi walikuja kote kote kutoka huko Winnipeg, Kanada, mpaka Costa Mesa, California. Nao wakafika kule, hawana hela, na huyo baba anasimulia jinsi ilivyombidi kumbadilisha nepi, mvulana mdogo mwenye umri wa kama miaka saba ama minane, hajiwezi kabisa. Na jinsi angeninii... hakuweza kupata nafasi ya kula wala cho chote kile, na akasema mvulana wake mdogo angeweza tu kumsikia akiongea. Naye angeweza kujua kwa kuangalia macho yake, ya

kwamba yeye alikuwa—alikuwa akijaribu kutabasamu, wajua. Na kujua ya kwamba yeye. . . Angeweza kumwambia mandhari mbalimbali aliyokuwa anaona, huko Marekani.

¹⁵⁵ Na wakati walipofika kule, California, walimwambia mfanyakazi katika idara ya usafiri, walichokuja kuona. Akasema, “Ati mmekuja kuona kitu gani cha Kiungu?” Na alama kubwa ya kuuliza.

¹⁵⁶ Bila shaka, mnaweza kuwazia kile Marekani ilichosema juu ya jambo hilo, mnaona. Mnaona, hao ni sisi, mnaona, “Sisi ni werevu sana! Tunajua kila kitu, unajua, na hakuna haja ya kutwambia cho chote. Tumeyaorodheshwa yote.” Mnaona?

¹⁵⁷ Kwa hiyo basi, kwa hiyo, “Ati kitu gani cha Kiungu? Ati mkaja kutoka huko mbali Winnipeg, Kanada?” Mbona, wao walifikiri jambo hilo lilikuwa ni baya sana.

¹⁵⁸ Hata hivyo, gazeti hilo likakodisha ga—gari likampeleka kule. Naye akawaambia, wakati walipofikia kwenye mstari, mahali ulipofikia, kasema watu elfu mbili mia saba walikuwa wakingojea kuombewa. Lakini kasema, walipomwona maskini mvulana huyo aliyelemaa, anayeonekana kama mtoto, na maskini baba yake huyo aliyevaa kofia, koti lake lililochakaa, kasema kila mtu alimpisha na kumpa nafasi. Alipofika jukwaani. . .

¹⁵⁹ Ni kinyume cha sheria kumpa mwingine kadi yako ya maombi. Mtu anapaswa kuja mkutanoni na kupata kadi yako mwenyewe. Kama ukishikwa mstarini, unabadilishana kadi na mtu mwingine, kadi hiyo ya maombi inakataliwa. Mnaona? Kwa sababu huna budi kuja kusikia maagizo na kujua jinsi ya kuupokea. Ni juu yako. Huwezi kumchukulia mtu mwingine. Huna budi kuja kulichukulia mwenyewe, kusudi upate kusikiliza. Mtu mkubwa fulani alisema, “Kama. . . Vema, siamini sana jambo hili. Lakini, labda kama Yeye ataniponya, mimi. . .” Mnaona? Na basi jambo hilo linasababisha fujo jukwaani, kwa hiyo wao wanaondosha tu jambo hilo kabla halijafikia mahali hapo.

¹⁶⁰ Kwa hiyo wakati mvulana huyo alipoanza, ama baba alipoanza kuja jukwaani, kuwatangulia hao watu, Billy alimwuliza kadi yake ya maombi. Hakuwa nayo. Kasema, “Kwa hiyo samahani, bwana.” Kasema, “Itakubidi ungojee.”

¹⁶¹ Akasema, “Vema.” Kasema, “Nitangojee.” Kasema, “Nitaingia tu kwenye zamu yangu kama hao wengine, basi.” Kasema, “Sikujua ilinibidi kufanya jambo hili.”

¹⁶² Na kwa hiyo nilikuwa nikizungumza na mtu fulani, ilitokea kwamba nilisikia hilo. Nilimwona baba huyo akiondoka, ndipo nikasema, “Kulikuwa kuna nini?”

Akasema, “Hakuwa na kadi ya maombi.”

Ndipo kitu Fulani kikaniambia, “Mrudishe.”

¹⁶³ Kwa hiyo nikasema, “Mlete hapa.” Ndipo yule baba akaja, huku majonzi yakitiririka usoni mwake, hajanyoa ndevu. Naye a—akaja, na hivi ndivyo *Reader’s Digest* ilivyosema. Mnaona? Sikumwuliza maswali yo yote, lakini niliangalia moja kwa moja usoni mwa mtoto huyo mchanga, nikamwambia mtoto huyo mchanga mahali alikotoka, kwamba alikuwa kwenye Zahanati ya Mayo, na yote kuhusu shida yake, jinsi alivyokuwa mgonjwa, na kila kitu.

¹⁶⁴ Na kwa hiyo huyo baba akaanza kulia, na akaanza kuondoka. Kisha akasema alianza kuondoka jukwaani, kisha akageuka, akasema, “Hiyo ni kweli, bwana.” Yeye Akasema, “Lakini je! mtoto wangu mchanga ataishi?”

¹⁶⁵ Nikasema, “Hilo siwezi kusema.” Nikasema, “Hebu kidogo.” Niliaona ono likitokea. Nikasema, “Hutapenda kuamini jambo hili, kwa sababu Mayo na Hopkins wote walisema kuwa upasuaji huo haungeweza kufanywa kwenye ubongo huo, lakini nitakwambia utakalofanya. Wewe, kesho, wewe nenda tu na mtoto huyu. Katika siku tatu zijazo utakutana na mwanamke mwenye nywele nyeusi barabarani, na mwanamke huyo atakuuliza huyo mtoto ana shida gani. Na ndipo atakwambia juu ya maskini daktari mmoja wa mashambani huku vijijini nje anayeweza kufanya huo upasuaji, nawe hutataka kuamini jambo hilo, sababu kwamba Mayo walikataa na kusema, ‘Hauwezi kufanyika.’ Lakini hiyo ndiyo nafasi pekee aliyo nayo mtoto wako, kupitia nguvu za Mungu, rehema ya Mungu na upasuaji huo. Sasa, kama unaniamini mimi kuwa nabii Wake, nenda ukafanye vile ninavyokwambia.” Kama kule kuweka zile tini juu ya Hezekia, na kadhalika.

Akasema, aligeuka na kusema, “Asante.” Akaondoka.

¹⁶⁶ Siku mbili ama zaidi zilikuwa zimepita, naye alikuwa yuko barabarani siku moja, ndipo mama mmoja akamwendea, akasema, “Mtoto wako mchanga ana shida gani?”

¹⁶⁷ Kasema, “Ana—ana ugonjwa wa ubongo.” Naye alikuwa anaendelea kuzungumza namna hiyo. Na, vema, wao—wao walifikiri ulikuwa ni mbaya sana, wajua.

¹⁶⁸ Kwa hiyo akasema katika dakika chache tu jambo fulani likatukia. Akasema, “Bwana, namjua mtu fulani anayeweza kumfanyia huo upasuaji.”

¹⁶⁹ Akasema, “Mama, angalia, Mayo Brothers walimkatia tamaa na kusema hauwezekani.” Kasema, “Mtu fulani hapa alikuwa anamwombea, anaitwa Ndugu Branham.” Kasema, “Amemwombea huyo mtoto.” Akasema, “Ngoja kidogo! Mwenye nywele nyeusi, amevaa suti la koti la kijivu.” Kasema, “Ni yeye.” Kasema, “Yuko wapi daktari huyo?” Naye akamwambia. Akampeleka kule na daktari huyo akamfanyia upasuaji, mtoto huyo akawa mzima.

¹⁷⁰ Sasa, hayo yalikuwa kwenye *Reader's Digest*, mnaona. Nao Mayo Brothers wakaniita kwenye mazungumzo kwa ajili ya jambo hilo. Kasema, “Kasisi Branham, ulimfanyia kitu gani mtoto yule?”

¹⁷¹ Nikasema, “Hakuna kitu. Sikumgusa hata kidogo. Nilisema tu yale Mungu aliyoniambia nimwambie. Mtu huyo akatii.”

¹⁷² Sasa, jambo la kushangaza juu ya jambo hilo, yapata majuma mawili baada ya jambo hilo, ama majuma mawili kabla ya jambo hilo, ama matatu, katika *Reader's Digest*, labda mwezi mmoja mbele yake, makala ya Bi Pepper yakatokea. Sasa, yeye ni mchawi halisi, ama kijumbe. Sasa, kuna aliye halisi, na kuna mtu fulani anayeiga. Wamekuwa na mwanamke huyo tangu 1897. Yeye ana zaidi ya miaka mia moja sasa, huko New York, ni ninii...kiziwi kama mlingoti. *Reader's Digest*, chukua... Nafikiri ilitokea kama miezi miwili ama mwezi mmoja baada ya yangu; nanyi mnaweza kuipata, miezi ya mwanzoni ya msimu wa kupukutika majani. Bw. Baxter alikuwa nayo hivi majuzi. Kama ningaliwazia jambo hilo, ningalimwambia... ama kama ningalijua ningesema jambo hili, ninge—ningalikuwa nayo. Ninaweza kuwaleteeni. Na ilitoa kama kurasa kumi ama kumi na nne. Yeye alikuwa tu mke wa nyumbani wa kawaida tu. Ndipo akapata jozi siku moja, wakati akiugua, naye akaanza kuzungumza na mizimu. Na wamemzungusha mwanamke huyo duniani kote, kila mahali. Walimpekeka Uingereza. Hata wakabadilisha nguo zake, mara nyingi, waone kama kulikuweko na makosa na kadhalika, na wakaenda kule na wakamfunika mtu usoni kwa kinyago, Myunani, na akajifanya kana kwamba alikuwa ni Mwingereza. Na mwanamke huyo akamwambia huyo mwanamume mambo yote. Naye alikuwa a— a—alitaka kumwita mmoja wa wenzi wake waliokufa.

¹⁷³ Sasa, jambo pekee ambalo huyo mwanamke...Kila mahali ulimwenguni, na hili hapa *Reader's Digest* ilichosema hapa, hapa siku chache zilizopita usiku, ama miezi michache iliyopita, moja ya mambo hayo yalifichuliwa wazi. Mtu fulani alidhaniwa anaubusu mkono wa roho ya mzimu wa mamaye, na kesho yake ilithibitishwa katika mahakama ya polisi ya kwamba alibusu tu kipande cha kitambaa cha jibini. Watu wengi sana wakiiga kijumbe! Wao ni hawa wasomaji wadogo wanaoketi kando ya barabara, ambao si vijumbe. Wao si kitu ila waigaji bandia. Lakini kuna kijumbe mwenyewe hasa.

¹⁷⁴ Nasi watu wa kidini, tuna waigizaji wengi sana pande zote mbili. Sasa tulieni kwa dakika chache.

¹⁷⁵ Sasa angalieni, ya kwamba huyo Bi Pepper ni kijumbe halisi. Na gazeti hilo lilisema, “Hapa pana jambo moja ambalo ni la hakika, ya kwamba, mtu anapokufa, yeye hajafa. Anaishi mahali fulani, kwa sababu mwanamke huyo anaita roho zao kuja kuzungumza na watu.”

¹⁷⁶ “Sasa, yeye anafanya nini, Ndugu Branham? Unaamini jambo hilo?” Naam, bwana. Biblia inasema hivyo, hiyo ndiyo sababu mimi ninaliamini. Naye ni wa Ibilisi. Ibada ya mizimu ni ujanja wa Ibilisi. Sasa angalia, sasa angalia hizo mbili.

¹⁷⁷ Na basi ungepaswa kuona barua zilizorushwa kwangu, wakati huo, hapo makala yangu yalipofuata yake. Je! si na ajabu ya kwamba, kabla tu ya wakati wa mwisho, Mungu alinena mambo haya? Na *Reader's Digest* linachapishwa katika kila lugha chini ya mbingu. Mnaona? Angalia, je! hivi si ni ajabu yalifuatana?

¹⁷⁸ Sasa hizi hapa barua zinakuja, kasema, “Ndugu Branham, hiyo inathibitisha ya kwamba wewe hu cho chote ila kijumbe.” Kasema, “Hiyo inathibitisha jambo hilo. Angalia, ulimwambia mwanamke yule mahali ambapo angepata... Mwangalie mwanamke *huyu*.”

¹⁷⁹ Nikasema, “Ngoja kidogo.” Nikatoa barua rasmi, (samahani) kuwatumia watu. Nikasema, “Ninyi wahubiri hamjui kitu.” Nikasema, “Badala ya kubatiza mwili wenu, mnahitaji akili zenu zibatizwe.” Hiyo ni kweli. “Hamkai mkayawazia mambo. Hamjaribu kuyawazia.”

¹⁸⁰ Hivyo ndivyo walivyofanya katika hizo siku za kale. Walimwona Yesu. Walijua Yeye aliweza. Alijua siri za mioyo yao. Alijua walilokuwa wakifanya namna hiyo. Nao wakasema, “Yeye ni mkuu wa pepo. Yeye ni Beelzebuli, mpiga ramli aliyezidi wote ulimwenguni.” Hawajakaa wakajaribu kuliwazia jambo hilo, kuona ya kwamba huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu. Hawakuwa wa kiroho vya kutosha kujua jambo hilo. Ndio hivyo, walisoma likawapita. Hakika, Yesu alipaswa kuja Yerusalemu, akiwa amepanda nyumbu, na kadhalika, bali wao walikuwa wakiangalia kule Kuja kwa mara ya pili.

¹⁸¹ Na ni jambo lile lile leo! Macho yao yanavuka jambo halisi. Haleluya! Hiyo ni kweli. Ninajua ya kwamba Mungu yupo hapa, alasiri ya leo, nami ninajua ninachukua wakati wenu mwingi sana, lakini hamna budi kuona jambo hili, rafiki. Kama sitapata kuwaona tena, hamna budi kujua pepo ni nini, hamna budi kujua Ukweli ni nini na uongo ni nini. Navyo vinafanana sana, huna budi kutenganisha kitu hicho.

¹⁸² Sasa kumbuka, haitakuwa ni huko nje, jambo fulani huko mbali sana upande *huu* kama wale Mafarisayo, ama jambo fulani kule nyuma upande *ule*. Jambo liko papa hapa mlangoni, papa hapa karibu nalo. Angalia. Sasa kama ningechukua...

¹⁸³ Hebu na tuchukue pande zote mbili. Kama ningechukua na kukupa dola, sasa, kama ningekupa dola ya bandia. Tutatumia mfano ili upate kuona. Jambo la kwanza ambalo ungefanya, kama wewe ni mtu mjanja, kama ukichukua dola na kuiangalia, jambo la kwanza, utaishikashika uone kwamba imetengenezwa kwa kitu gani. Hiyo ni kweli? Utaangalia

imetengenezwa kwa kitu gani. Utaangalia thamani yake. Dola halisi haikutengenezwa kwa karatasi, ni karatasi kwa sehemu na hariri kwa sehemu, unaona. Na jambo la kwanza, huna budi kuangalia thamani yake. Hicho ndicho kidokezo cha kwanza.

¹⁸⁴ Na sasa hebu na tumweke mwanamke huyo upande *huu*; na tumweke Bwana upande *huu*, ambaye anatenda kazi pamoja nasi.

¹⁸⁵ Sasa angalia, jambo la kwanza unalopaswa kuangalia, kila kitu. . . Angalia makala yako. Katika miaka hamsini-na-kitu ya kupiga ramli, na kupandisha roho za waliokufa, hata mara moja hajamtaja Mungu, Kristo, uponyaji wa Kiungu, ukombozi, Hukumu, wala cho chote kile. Hakuna kitu ila mizaha na upumbavu ndani yake.

¹⁸⁶ Lakini upande *huu*, wakati wote ni Mungu, Hukumu, Kuja kwa Yesu, Uponyaji wa Kiungu, nguvu za Mungu, ukombozi. Angalia thamani yake. Huwaoni wapiga ramli na wachawi huko nje wakihubiri Injili. Watu wana nini? Jamani! Angalia!

¹⁸⁷ Na jambo halisi la kufanya, kama ukitaka kujua kama ni dola halisi ama la, kama inafanana sana nayo, chukua namba zake uzipeleke kwenye kiwanda cha sarafu. Na kama kuna namba kule ambazo zinaambatana na hizo, kuna dola ya fedha inayoingojea. Hiyo ni kweli?

¹⁸⁸ Vema, basi, ndugu, chukua aliyofanya yule mwanamke na uyarudishe kwenye Biblia, utaona ya kwamba ni yule mchawi wa Endori.

¹⁸⁹ Nawe chukua kile kilicho hapa, utakiona kimerudi, kiko kwenye kitabu hapa kwenye kile Kiwanda, “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Bila shaka, kazi Zake zile zile! Yeye hakwenda na kufanya upumbavu na upuuzi na watu. Ilikuwa kwa ajili ya manufaa fulani, kumsaidia mtu fulani, kuwaongoza kwa Mungu. Amina! Mimi sijisemei “amina” mwenyewe, lakini *amina* maana yake ni “na iwe hivyo.” Nami ninaninii. . . Ninaamini jambo Hilo. Ninajua ni Kweli.

¹⁹⁰ Sasa angalia, hili hapa. Sasa, upesi sasa, maana sitaki kuwaweka zaidi.

¹⁹¹ Hapa, hebu na tuchore picha hapa, picha ndogo ya akilini. Hiki hapa kijito kinachopitia hapa, kinaenda moja kwa moja upande *huu*, kikipitia katika maisha. Sasa angalia. Ni mfereji. Nisikilizeni kwa makini sana sasa, ili msilikose jambo hili. Moja kwa moja kushuka chini namna *hii*. Sasa, katika mfereji *huu* hapa wanaishi wanadamu, mimi na wewe. Sasa, ndani mle, hebu tuone ni kitu gani. Ni upuzi mtupu na kila takataka, lakini mara kwa mara utaona nuru. Unaona giza na barabara, hayo ni makelele na shangwe, pepo wakiwapagaa watu. Loo, wanavaa vizuri, jamani, na ni waungwana wawezavyo kuwa, wasomi wa hali ya juu, lakini angali ni Ibilisi. Lakini kuna waliozaliwa mara ya pili wameketi pale.

¹⁹² Sasa, watu hawa kwenye mfereji huu wanashawishiwa kutoka pande mbili mbalimbali. Sasa, upande huu kuelekea *huku*, kuna utatu. Na upande huu kuelekea *huku* kuna utatu.

¹⁹³ Sasa, wakati, sasa kwanza, upande *huu*, ni nafsi za *wasio haki*, wakati mtu anapokufa anaenda mahali anapongojea hukumu. Yesu alienda akazihubiri nafsi zilizokuwa kifungoni kule. Unaofuata ni pepo. Unaofuata ni Ibilisi na kuzimu. Ukipanda juu, wa kwanza, sasa, hao huko ni vizuka, roho za waliokufa, watu wasiotubu hata. Wao wanangojea ile Hukumu. Jambo pekee wanalojua ni upumbavu na yale waliyofanya.

¹⁹⁴ Sasa, hapa juu, hawa Wakristo wanashawishiwa kutoka Juu. Huu ni mfano. Hapa juu ni Roho, mwingine, Roho Mtakatifu, Roho wa Mwanadamu, Yesu Kristo. Roho Mtakatifu, Roho Mtakatifu hulishawishi Kanisa Lake katika mazingira haya ya wanadamu.

¹⁹⁵ Ibilisi, kwa roho *hizi*, anamshawishi mwanadamu. Sasa, angalia, kinachofuata ni malaika. Halafu ni Mungu. Sasa, kila mwanadamu hapa anashawishiwa na moja ya dunia *hizi*. Mnaona ninalomaanisha?

¹⁹⁶ Sasa kile alichofanya mwanamke huyo, aliingia katika ulimwengu huo. Naye anazungumza na hao wanaume waliopagawa na pepo ambao walikuwa, hapo mwanzo, roho za hao malaika walioanguka ambao hawakutubu kule nyuma hapo mwanzo, nao wakaachilia miili yao ipagawe nao. Nao wanangojea ile Hukumu.

¹⁹⁷ Na *hawa* hapa wanashawishiwa na kuzaliwa mara ya pili na Roho wa Mungu. Naye Ibilisi ana manabii wake, na Mungu ana wake. Mnaona ninalomaanisha? Ni ushawishi, hebu na twende. Simama upate kuwatenganisha. Yesu, alipokuwa hapa duniani. . .

¹⁹⁸ Sasa, leo, hawezi kuingia katika ulimwengu huo na ampate mwenye haki kutoka katika ulimwengu ule. Asingeweza kufanya jambo hilo, maana wenye haki hawamo humo walimokuwa wakikaa, Paradiso. La bwana, Paradiso iliondoshwa, wakati Damu ya Yesu ilipoiondolea mbali. Angalia hapa. Jamani!

¹⁹⁹ Kama ningaliweza kufikiria jinsi ambavyo Yesu, wakati alipokufa, alienda akawahubiri nafsi waliokuwa kifungoni. Yeye alikufa, mwenye dhambi, asiyejua dhambi, hata hivyo dhambi zetu zilikuwa juu Yake. Na Mungu, kwa ajili ya dhambi Zake, akamtupa kuzimu. Biblia ilisema, "Alienda akazihubiri hizo nafsi."

²⁰⁰ Baadhi ya watu husema, "Ndugu Branham, siwezi kuelewa na jambo hilo." Wamesema, "Yesu alifufuka siku ya tatu. Yeye alikufa Ijumaa alasiri na kufufuka Jumapili asubuhi, mbona, Yeye alikuwa amekufa siku moja tu."

²⁰¹ Yeye alisema, “Katika kipindi cha wakati huo,” kwa kuwa alikuwa na Andiko moja katika Biblia, ambalo angaliweza kusimamia. Kwa kuwa, Daudi, mtu aliyerudi nyuma baadaye, lakini alikuwa ameokoka, lakini akiwa ni nabii chini ya upako wa Mungu, alisema, “Sitakuachia kuzimu nafsi Yake, wala sitamtoa Mtakatifu Wangu aone uharibifu.” Naye alijua, siku tatu usiku na mchana, ya kwamba mwili huo ungeanza kuoza. Naye Mungu alikuwa tayari amemwambia nabii, “Hataona uharibifu.” [Sehemu tupu katika kanda—Mh.]

Haleluya! Yeye alichukua Neno la Mungu. Akamshinda Shetani, kila wakati, Kwalo. Alishinda mauti, kwa Neno la Mungu. Haleluya! Alishinda mauti. Na wakati walipomwua, Naye akafa, mwenye dhambi, dhambi zangu na dhambi zako zilikuwa juu Yake, alishuka, naweza kumwona akipiga hodi mlangoni pale.

Ndipo hizo nafsi zilizopotea zikatoka na kusema, “Je! U nani Wewe?”

²⁰² Akasema, “Mbona hamkumsiliza Henoko? Mbona hamkuwasikiliza wale manabii waliohubiri?” Walihukumiwa. “Mimi ni Mwana wa Mungu ambaye wakati mmoja nilikuwa hai. Mimi... Damu Yangu imemwagika. Ninakuja kuwaambieni, nilitimiza yale manabii waliyosema nitatimiza.” Akashuka moja kwa moja kuwapita pepo, akaingia moja kwa moja kuzimu, akazinyakua funguo za mauti na kuzimu kutoka kwa Ibilisi, akazining'iniza ubavuni Mwake, akaanza kupanda. Haleluya!

²⁰³ Kunapambazuka. Haleluya! Hebu tuchore picha ndogo hapa. Asubuhi na mapema, kulikuweko na kundi lingine lililokaa hapa Paradiso. Hawako huko sasa.

²⁰⁴ Sasa, enyi marafiki wakubwa Wakatoliki ambao mnaamini katika kuombewa na watakatifu. Kama mnazungumza na mtakatifu fulani kanisani mwenu, mtu huyo ni mwenye dhambi, yuko kuzimu, ama—ama anangojea hukumu yake. Na kama yeye alikuwa mtakatifu, yeye yuko katika utukufu wa Mungu wala hawezi kurudi. Hiyo ni kweli. Ninaweza kuthibitisha jambo hilo. Ile damu ya mafahali haingeiondoa dhambi, lakini Damu ya Yesu ilitaliki dhambi.

²⁰⁵ Ninaweza kumwona Yesu akiedna kule ambako, Paradiso, kuna mzee Ibrahimu, Isaaka na Yakobo, na hao wengine kule, Samweli na hao wengine wote kule. Ninaweza kumsikia akipiga hodi mlangoni. [Ndugu Branham anagonga mimbarani mara sita—Mh.] Amina! Loo, ninapenda jambo hili. Ninajisikia furaha... ninajisikia wa kidini kwa namna fulani sasa. Ninaweza kumwona Yeye akiangalia kule. Ninaweza kumsikia akisema, “Ni nani yuko hapo nje? Wewe ni nani?” Akasema, “Mimi, huyu ni Ibrahimu anazungumza. Wewe u nani?”

206 “Mimi ni Mzao wa Ibrahimu.” Amina. Ninaweza kumwona Ibrahimu akija mlangoni, anafungua mlango. Akasema, “Mimi ni Mzao wa Ibrahimu.”

Danieli alisema, “Angalieni kule! Yule ndiye lile Jiwe nililoona limekatwa toka mlimani bila kazi ya mikono.

207 Ninaweza kumsia Ezeieli akisema, “Yule pale! Nimemwona, kama mavumbi chini ya miguu Yake, mawingu yanasogea, wakati kondoo dume... walipopiga makofi, majani, na wote wakapiga makelele.” Loo, ninaweza kuona watu mbalimbali kule Paradiso, wakimngojea.

208 Ninaweza kumsikia akisema, “Njoni! kunapambauka huko Yerusalemu. Hatuna budi kutoka hapa. Tunapaa kwenda juu, kwa sababu mlitumainia damu ya mafahali na mbuzi, mkingojea wakati wa Damu Yangu. Lakini damu Yangu imemwagika kule juu Kalvari. Mimi ni Mwana wa Mungu aliyefanyika mwili. Madeni yote ya dhambi yamelipwa. Tuko safarini tukitoka!” Haleluya! Mungu atukuzwe!

209 Ninaweza kumwona Ibrahimu akinyakua mkono wa Sara, na hapa wanakuja, wanatoka kabisa! Katika Mathayo 27, wakati alipotoka, naweza kuwasikia wakisimama kidogo hapo Yerusalemu. Na muda si muda mwajua, naweza kumwona Kayafa na hao wengine wamesimama barabarani, wakisema, “Wao wananiambia ati huyo jamaa alifufuka. Aisee, ni jamaa nani yule anayeenda kule; kijana yule, yule msichana mdogo?”

210 Si wazee tena; hao walikuwa ni Ibrahimu na Sara. Nao wakatoweka. Wakaangalia, “Mtu fulani anatuangalia.” Waliweza kutoweka kama tu vile alivyopitia kwenye ukuta, mwili wa namna ile ile. Haleluya! Kweli. Hawa hapa manabii wote na hao wengine, wakitembea kila mahali, wakiuzuru ule mji.

211 Naye Yesu akawaongoza juu moja kwa moja na kuingia ndani, ama juu kupitia kwenye nyota, mwezi, mawingu, na kuwaongoza mateka alioteka, akawapa wanadamu vipawa. Yesu anaketi leo katika mkono wa kuume wa Baba, alipanda kule juu, akaketi chini, mpaka adui Zake watakapowekwa chini ya miguu Yake.

212 Na siku hizi, rafiki yangu Mkristo mpendwa, pepo wanatenda kazi kila mahali. Naye Roho wa Mungu anatenda kazi wakati wote, kwa upande mwingine, kukabiliana naye kila wakati. Haleluya! Ndivyo ilivyo. Magazeti ya kila siku na ya kipindi kwa kipindi na cho chote kile yanatangaza jambo hilo. Wanaliangalia. Hayawezi kuona ni kitu gani. Ni kitu gani? Ni utangulizi wa shindano kubwa la kuamua linalokuja karibuni sana, kati ya Mungu na Ibilisi. Ingia upande wa Mungu na uwe sawa moyoni mwako. Amina.

213 Hapa si muda mrefu uliopita nilikuwa kule Toledo, Ohio, nikifanya mikutano. Naenda kufunga.

214 Mnaona ninalomaanisha kuhusu pepo? Wanafanya kazi. Ni wa kidini sana, wa kidini kama ninii! Loo, yanaenda kanisani kila Jumapili, yanakariri Imani ya Mitume, na kuimba Nyimbo za Sifa. Loo, jamani, wa kidini tu jinsi wawezavyo kuwa!

“Ndugu Branham, unamaanisha hayo ni Kweli?”

215 Hiyo ndiyo aina ya roho iliyokusulibisha Yesu Kristo msalabani. Na Yesu alisema, “Ninyi ni wa baba yenu, Ibilisi.”

216 Sasa baadhi yao walisema, “Loo, Urusi ni mpinga-Kristo.” Hata kidogo! Urusi siye mpinga-Kristo. Mpinga-Kristo atakuwa wa kidini sana hata itawapumbaza walio Wateule kama yamkini.

Kumbukeni, Mungu huchukua mtu Wake, lakini kamwe si Roho Wake. Ibilisi huchukua mtu wake, lakini kamwe si roho yake. Sasa, hizo hapo. Jichagulieni. Mimi ninawajibika na kusema Kweli tu.

217 Pepo, wakitenda kazi! Jana, nilikuwa nao katika ulimwengu wa kimwili. Leo, ninawaonyesha katika ulimwengu wa kiroho, ambapo wako kwenye ulimwengu wa kidini. Ambapo wako kule, wanaitwa kansa, nao wanayaita *hivi*, *vile*, na *vinginevyo*, lakini nimewathibitishia, kwa Biblia, ni pepo. Sasa, upande huu, leo, hawa hapa tena katika ulimwengu wa kidini, ni wa kidini sana, watawa.

218 Kama utanza, ndugu, na uwazie. Kaini, mwanzo kabisa wa jambo hilo, alikuwa ni mtu wa kidini sana. Esau alikuwa ni mtu wa kidini sana. Yuda alikuwa ni mtu wa kidini sana. Ni dini. Si ulimwengu wa nje. Ni mumo humo miongoni mwenu. Angalieni jambo hilo, elimu juu ya pepo! Labda baadaye kidogo, wakati mwingine, ninaweza kuliingilia zaidi. Tunachelewa sana.

219 Usimhukumu mtu ye yote. Mpende kila mtu. Kama huwezi kupenda kwa moyo wako, basi Kristo hayuko nawe.

220 Huko Toledo, Ohio, niliingia katika mkahawa mdogo. Nilikuwa nikila mahali fulani, mahali fulani pa Dunkard, mahali pazuri sana padogo. Walikuwa ni watu wazuri sana. Alasiri hiyo walikuwa wamefunga, wapate kwenda kwenye shule ya Jumapili. Na wakati walipoondoka kwenda, ilinibidi kuvuka barabara, kwenda kwenye mahali fulani pa zamani pa kilimwengu, nami nikaingia hapo. Nami ninajua si halali kucheza kamari huko Ohio. Na hapa alisimama Polisi Mzalendo amekumbatia msichana, mkono wake ukining’inia hapa kifuani mwake, akicheza na chombo cha kucheza kamari. Sheria ya nchi yetu na taifa letu, vimekufa vyote. Ni jambo la kuhuzunisha!

221 Mimi ninamtumaini Kristo Mwamba wenye imara, ninasimama, mahali pengine po pote ni mchanga unaodidimilia. Hakuna kingine kilichosalia. Hiyo ni kweli.

222 Niliangalia kule nyuma, na kulikuweko na maskini msichana mmoja mzuri, labda kwenye umri wa miaka kumi-

na, kumi na tisa, kumi na nane, umri wa miaka kumi na tisa. Na yale waliyokuwa wakifanya, hao wavulana kule nyuma ya ile meza, yalikuwa ya kutisha. Nikaketi pale. Na sasa nilishangaa, nimeketi papa hapa ambapo mama mmoja alikuja, akasema, “Ungependa kuketi?”

Nikasema, “Asante. Nilitaka kifungua kinywa.”

²²³ Nami nikiwa nimeketi kwenye kiti, hapa aliketi mama mzee, rika la mama yangu, umri wa miaka hamsini na mitano, hamsini na minane. Alikuwa amevaa jozi ya maskini hizo nguo fupi chafu wanazovaa.

²²⁴ Wanadai ni joto. Sayansi inasema, “Una kichaa.” Bila shaka, si joto. Unataka tu kujionyesha uchi wako. Ni aibu, fedheha. Mwanamke wa heshima hawezi kuzivaa. Mwanamke atazivaa, lakini mama wa heshima hawezi.

²²⁵ Halafu, kwa hiyo basi wao...huyo hapo, ameketi pale. Maskini mwili wake ulikuwa debwedebwe. Alikuwa amejipaka vipodozi vya makucha vya rangi ya maua, cho chote unavyoviita, mdomoni. Na kukata nywele zake kama mwanamume, ule mtindo wa kimbimbi; vile ilivyosema Biblia, jambo ambalo lilikuwa ni fedheha. Na mwanamke, kwamba mwanamume...

²²⁶ Biblia inadai, kama mwanamke akikata nywele zake, mwanamume ana haki ya kumwacha kwa kumtaliki, kwa sababu yeye si mwaminifu kwake. Inatubidi tushuke tuje tuhubiri Biblia hapa moja ya siku hizi. Ilisema, “Kama akikata nywele zake, yeye anamwaibisha mumewe.” Kama yeye ana dharau, anapaswa kutalikiwa. Huwezi kuoa mwingine, lakini anaweza kumtaliki. Whiu! Jamani, hilo, hilo linaudhi, naweza kulihisi. Lakini hiyo ni Kweli.

²²⁷ Loo, ilikuwa kwamba, tulikuwa na jambo hilo katika ulimwengu wa Roho Mtakatifu, lakini tukaachilia mlango wazi. Maskini ndugu wa kale alizoea kusema, “Tuliacha milango wazi, tuliacha mlango wazi, tukapatana na dhambi. Tuliacha mlango wazi, kondoo wakatoka, lakini mbuzi waliingiaje?” Mliacha milango wazi. Hiyo ndiyo iliyokuwa shida. Mliacha milango wazi, ulimwengu na kanisa vikachanganyikana. Kama vile tu Wamoabu na kadhalika, na Balaamu, na jinsi alivyooa miongoni mwao, hilo ndilo jambo lile lile leo. Na kanisa lote limechafuliwa, na wakati wa Kipentekoste ndio wakati wa Laodikia, ambao unakuwa vuguvugu, na kutapikwa kutoka katika kinywa cha Mungu. Na kutoka katika kundi hilo lote, Mungu anaita waliosalia, na kuwapeleka Nyumbani, hiyo ni kweli kabisa, kupitia ufufuo.

²²⁸ Na huyo mama alikuwa pale, ameketi pale, amejaa rangi ya midomo usoni mwake mwote, na ilikuwa imeenea mahali namna hiyo. Naye alikuwa na kitu hiki cheusi kwenye macho yake, na alikuwa anatoka jasho, lilikuwa linatiririka. Na maskini kizee cha watu huenda kilikuwa na vitukuu. Naye alikuwa

ameketi pale na wazee wawili, na mmoja wao alikuwa na shali kubwa shingoni mwake, na ni mwezi wa Juni, ameketi pale. Naye akasimama, naye alikuwa anakunywa pombe, na huyo mwanamke naye alikuwa anakunywa pombe, pia. Akiangalia huku na huko.

²²⁹ Nikawazia, “Ee Mungu! Mungu, kwa nini usiondoe kitu hiki kutoka kwenye ramani? Mbona usikiondolee mbali? Je! mtoto wangu Sharon... Mtoto wangu mchanga, mtoto wangu Sarah na mtoto wangu Rebekah kulelewa katika kizazi hicho kuja kukutana na upuuzi kama huo?” Nikawaza, “Angalia hapa nje katika bustani hizi na kadhalika, na yale yanayoendelea.” Nikawaza, “Ee Mungu! Loo, ninafurahi ya kwamba ulimchukua Sharon kama yalikuwa ni mapenzi Yako. Je! Maskini mtoto wangu Rebekah na mtoto—mtoto Sarah itawabidi kulelewa katika upuuzi kama huo?” Ambapo, na hao watu wanaiita... wanaimba katika kwaya na kila kitu. Ndipo nikawaza, “Je! si ni aibu hiyo?” Nikawaza, “Mungu, haki Yako inawezaje kustahimili jambo hili? Inaonekana kama kwamba hasira Yako yenye haki ingeruka kule na—na kupalipua mahali hapa.”

²³⁰ Ndipo nikamsikia Malaika wa Bwana, akasema, “Sogea huku.” Nikaenda pale. Na wakati alipomaliza nami, nilijisikia kana kwamba ni mtu tofauti. “Kwa nini unamhukumu?”

Nikasema, “Angalia pale, jinsi alivyo.” Na haya ndiyo Yeye...

²³¹ Nikaona ono. Nikaona ulimwengu namna *hii*, mviringo, ulimwengu mwingine. Lakini ulimwengu huu *hapa*, ulikuwa umezungukwa na upinde wa mvua, na hiyo ilikuwa ni Damu ya Kristo ambayo huzuia hasira ya Mungu. Yeye hangeangalia hiyo, Yeye—Yeye angeangamiza kitu hicho mara moja sasa hivi, kwa sababu Yeye alisema, “Siku mtakayokula kutoka kwake, siku hiyo mtakufa.” Kwa hiyo Yeye angefanya jambo hilo.

²³² Ndipo nikawazia namna *hii*. Nilijiona mimi mwenyewe. Ingawa nilifikiri sikutenda hayo, lakini nilikuwa mwenye dhambi, hata hivyo. Halafu Damu ya Yesu Kristo inatenda kazi kama kinga kwetu. Unaona? Hivi kwamba, ninapotenda dhambi, dhambi zangu humgusa Yeye na kukikwaruza kichwa Chake cha thamani, nami ningeweza kuona machozi na Damu vikitoririka. “Msamehe, Baba, hajui analotenda.” Kisha ningefanya jambo lingine na linakipiga kichwa Chake. “Msamehe, Baba.”

²³³ Kama ingeliwahi kumpita Yeye, ningeliangamizwa. Na kama sikuwa nimekubali neema Yake, na ile siku nafsi yangu itakapoabiri ipite hapo, tayari nimekwisha kuhukumiwa. Nimekataa. Hakuna jambo lililosalia ila hukumu. Kwisha hukumiwa, tayari nimekwisha kuhukumiwa. Mungu alisema, “Siku utakayokula, siku hiyo utakufa.” Unahukumiwa kwa haki. Hiki ni kiti cha hukumu alasiri ya leo, msimamo wako kumhusu Kristo.

²³⁴ Ndipo nikawazia, “Naam, hiyo ni kweli.” Nami nikaona siku moja nilitambaa nikaenda Kwake. Niliona kitabu changu cha kale kimewekwa pale, mwenye dhambi, kila kitu kiliandikwa mle. Niliona dhambi zangu ndizo zilizokuwa zinasababisha jambo hilo, ndipo nikasema, “Bwana, utanisamehe?”

²³⁵ Akaweka mkono Wake ubavuni Mwake, akatoa Damu kidogo, akaandika hapo juu, na kusema, “Amesamehewa.” Akakitupa katika bahari ya usahalifu, zisikumbukwe tena. Zimetoweshwa milele! Akasema, “Ninakusamehe, lakini unamhukumu.”

Hilo lilibadilisha wazo langu. Nikasema, “Bwana, nirehemu.”

²³⁶ Baada ya mimi kutoka kwenye hilo, nilienda pale na kuketi. Nikasema, “U hali gani, mama?”

Akasema, “Loo, aloo.”

²³⁷ Nami nikasema, “Samahani,” nikasema, “Mimi ni Kasisi Branham, mhudumu.”

Akasema, “Aa, samahani. Samahani, Kasisi Branham.”

²³⁸ Nikasema, “Mama.” Nikamwambia yaliyotukia. Nikasema, “Nilikuwa nimesimama pale, nami nilikuwa nikikuhukumu, na kuwazia, ‘Ni jambo baya namna gani!’ Labda una watoto.”

Akasema, “Ninao.”

²³⁹ Nikasema, “Kitu gani kilisababisha mambo kwenda mrama?” Akaanza kunihadithia hadithi ambayo ingeurarua moyo wa cho chote kile. Nikasema, “Ni—nilikuwa nikimwuliza Mungu kwa nini Yeye hakuangamiza mambo hayo kutoka katika nchi. Hapa, wewe hapa pamoja na hawa wanaume wawili walevi, nawe mwenyewe umelewa, wewe mwenyewe.” Nikasema, “Siku moja... Damu hiyo inakuzuilia hasira ya Mungu. Utakufa moja ya siku hizi. Na, ndipo, wewe—wewe ni mtu mwenye hiari ya kujichagulia sasa, unaweza kukataa ama upokee.” Nikasema, “Lakini siku moja nafsi yako itavuka huko ng’ambo, ambako hakuna rehema iliyosalia. Na kama ukifa katika dhambi zako, wewe tayari umehukumiwa, na unaenda kuzimu.”

²⁴⁰ Unajua nini? Mwanamke huyo aliondoka kwenye kiti hicho pale kwenye ile hoteli. Tulikuwa na mkutano wa maombi ambao hujawahi kuusikia maishani mwako, ndipo akamjia Kristo. Ilikuwa ni nini? Usiwahukumu; waambie Injili. Wao wamepagawa na pepo; wao ni wanadamu katika ulimwengu huu. Wanashawishiwa kutoka upande huu. Ushawishi wetu unatoka juu. Hebu tuone tunachoweza kufanya na talanta zetu, kuwaleta watu kwa Kristo.

²⁴¹ Baba yetu wa Mbinguni, tunakushukuru kwa ajili ya wema Wako na rehema. Ninasikitika, Bwana; labda, hawa watu, nimewaweka hapa muda mrefu sana. Lakini kwa kuwa ndio

kumalizia kwa hii mikutano ya alasiri kama huu, nilitaka kuwaambia, “pepo,” nami nilikata mengi yake sana katika mahali pamoja, katika somo moja, lakini labda wanaweza kulipata, hapa na pale, na kufahamu kile nilichomaanisha. Unajua kusudi la moyo wangu, wa kulileta.

²⁴² Naomba watu waondoke hapa alasiri ya leo, na wanaume na wanawake waangalie kila hatua wanayopiga, lakini waishi wenye furaha na huru. Jalia wajue ya kwamba Mungu aliwaokoa. Pia jalia wamtazame Yeye, wasahau itikadi zote na vitu vilivyowazunguka, na waishi kwa amani na kwa kiasi, na katika kumcha Mungu. Na halafu, Mungu, unapotaka kuwatumia kwa jambo lo lote, Wewe unaweza kusema nao moja kwa moja na kuwatuma ko kote unakotaka waende ama lo lote unalotaka wafanye. Naomba ya kwamba watu wawe wanyenyekevu na wampate Kristo mioyoni mwao. Tusamehe, Bwana, kwa makosa yetu, kila mmoja wetu.

²⁴³ Nasi tunajua ya kwamba—kwamba Shetani ametoka akizunguka-zunguka kama simba anayenguruma, kila mahali, akiwala wale anaoweza, wakivaa mavazi ya dini. Ee Mungu, maskini watoto hawa wachanga, waangalie, kila mahali. Wametupwa na kuachwa katikati ya watu. Nami nakuomba, Mungu, uwarehemu, na uokoe wote waliopotea, waponye wagonjwa. Pia, Mungu, tunatambua ya kwamba pepo hawa wachafu wa maradhi wanaowajilia watoto Wako, ambao una upatanisho ulio huko ng’ambo, utakaoshughulikia jambo hilo. Na pepo wote ambao wangewafanya kutenda dhambi, una upatanisho uliowekwa kule, utakaoshughulikia jambo hilo. Nami naomba ya kwamba utatujalia hayo katika Jina la Yesu. Amina.

Sijui kama kuna . . .



Elimu Juu ya Pepo — Milki ya Kimwili

8 Juni, 1953, Jumatatu alasiri

Roberts Park Amphitheater, Connersville, Indiana

Elimu Juu ya Pepo — Milki ya Kidini

9 Juni, 1953, Jumanne alasiri

Roberts Park Amphitheater, Connersville, Indiana

Roho Zinazoshawishi

24 Julai, 1955, Jumapili asubuhi

Maskani Ya Branham, Jeffersonville, Indiana

Jumbe hizi za Ndugu William Marrion Branham, zilizohubiriwa hapo awali katika Kiingereza, zimetolewa kwenye kanda za sumaku zilizorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2001 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org